# DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE

## 1. Mke Wangu

⇒ Anwani inaweka msisitizo katika sifa ambazo msimulizi angetaka mke wake awe nazo na tabia za mke aliyemuoa.
⇒ Mkewe ana pingana naye hatimaye anaomba talaka.

**Maudhui**

**Migogoro**

⇒ Msimulizi hafanyi kazi na anawategemea wazazi. Aziza haoni mtu asiyefanya kazi kama mume wake.
⇒ Kuhusu kutumia mswaki na burashi, viatu na msimulizi kutotaka muuza madafu aingie ndani.

**Ushamba na ujiji**

⇒ Aziza kutovaa viatu, kutotumia burashi na dawa ya meno na badala yake mswaki na unga.

**Utamaaduni**

⇒ Wazazi wa msimulizi japo ni matajiri wanashikilia utamaaduni wa kuwachagulia watoto wachumba au wake.
⇒ Msimulizi hataki kumwoa Salma Fadhil kwa utamaaduni wake wa kuificha sura yake kwa kuiremba marangi ya mAshavu na midomo.
⇒ Utamaaduni wa mume kufanya kazi aweze kukimu familia.
⇒ Utamaaduni wa mavazi/vifaa-viatu, mswaki, unga.
⇒ Msimulizi na hata Fedhele wameacha mila na kugeukia uzungu. Fedhele anavaa kanzu inayomfika mapajani.
⇒ Uigaji wa utamaaduni wa kigeni huweza kuwaathiri wanawake kwa kuwakosesha waume wa kuwaoa kama Fedhele.
⇒ Kuoa watu wenye uhusiano wa damu nao-wazee wa Seluwa mtoto wa shangazi walitarajia msimulizi amuoe.

**Ukandamizaji wa wanawake/taasubi ya kiume**

⇒ Msimulizi kusema 'Huyu ni mwanamke na wanawake ni kama watoto wadogo, hawaachi kisebusebu.
⇒ Msimulizi anataka kumwoa mwanamke mshamba amstaarabishe kuonyesha anachukulia mwanamke ndiye anahitaji maongozi ya mwanamme ilhali ni kinyume.
⇒ Kumdharau Fedhele kwa kutembea usiku wakiwa pamoja na mvulana ni kuchukulia wanawake kama vyombo visivyoweza kujidhibiti.

**Heshima na utiifu**

⇒ Aziza hana heshima kwa mumewe kwani Anamkashifu, anamuumbua na kumzungumzia kwa ujeuri, kejeli na hata akiwa ametoa macho. Anasema ni upuzi kukaa, kuchana nywele na kutembea.
⇒ Msimulizi anamweshimu mkewe kwani licha ya kejeli na ukaidi wake, anamjibu kwa upole na kumruhusu aseme. Anaona kuwa kumwamrisha mkewe lazima kungemshinda-busara.

**Kazi na athari za kuikosa**

⇒ Msimulizi anadharau kazi za mikono kwa kusema angeonekana wazimu akichoma mihogo.
⇒ Kazi ni muhimu kwa kila binadamu hata awe wa tabaka gani.
⇒ Kukosa kazi kunamwathiri msimulizi kwa kumkosesha mkewe ambaye amchukulii kama mumewe kwa kuwa hafanyi kazi bali anaishi kwa jasho la wengine-wazazi na mtumishi mapanya.

**Utabaka**

⇒ Kuna matajiri/makabaila (wenye nacho) kama vile msimulizi na wazazi wake na maskini/makabwela (wasionacho) kama vile wazazi wa aziza, mapanya na muuza madafu.
⇒ Matajiri wanaishi kwa jasho la maskini wanaofanya kazi ngumu.
⇒ Watu wa daraja la juu wanaishi mijini na wa daraja la chini shambani.
⇒ Watu wa tabaka la juu wameelimika ilhali wale wa tabaka la chini hawajaelimika kama vile Aziza.
⇒ Watu wa tabaka la juu wanafanya kazi za ofisi na wa la chini kazi za mikono kama vile ukulima, kuchoma mihogo na kuuza, kukwea minazi na kuuza madafu.

**Ustaarabu**

⇒ Watu wa mjini wanachukuliwa wamestaarabika na wa shambani hawajastaarabika. Kinaya ni kwamba yanayodaiwa ni ustaarabu ni kupuuza utamaaduni asili na kuiga ule wa kigeni.

**Ndoa**

⇒ Ndoa ya msimulizi inavunjika kwa kukosa kazi.
⇒ Za wengine wa mijini zinavunjika kwa wanaume kutaka kuwadhibiti wake au kuwatoa mambo ya kilimwengu.
⇒ Ndoa huathirika ikiwa watu hawana mtazamo na mwelekeo mmoja.
⇒ Ndoa za matabaka tofauti zaweza kuingia doa

na kuvunjika. Unaweza kumtoa mtu shambani ilhali huwezi kutoa ushamba ndani yake.

**Elimu**

⇒ Humkomboa mwanamke kutokana na udhalilishaji wa mwanamume kwa vile inamwongezea mwanamke hadhi na hata kufanya mwanamume amwogope.

⇒ Huwafanya watu kuwa watumwa kama vile kuwafanya wadharau kazi za mikono au kujiajiri wenyewe na kutaka tu kuajiriwa ofisini-uboi wawe wakitumwa.

⇒ Yaweza kupotosha watu na kuwasahaulisha mila na desturi zao.

**Ukengeushi**

⇒ Msimulizi ambaye amesoma kumwoa mwanamke ambaye hajasoma.

**Ujasiri**

⇒ Aziza kumkabili mumewe na kumwambia ukweli bila kuogopa angepigwa au kutalikiwa.

**Udhabiti wa msimamo**

⇒ Aziza kukataa kutumia burashi, dawa ya meno na viatu.

⇒ Kutaka mume anayefanya kazi na anapotambua sivyo msimulizi alivyo anaamua kumtaliki na kufuata ndoto yake.

**Nafasi ya mwanamke katika jamii**

⇒ Msomi kama vile wa mjini.

⇒ Ananyimwa elimu kama vile wa shambani.

⇒ Ana uhuru kama vile Fedhele.

⇒ Anathamini kazi na kuichukulia kama kipimo cha utu.

⇒ Ana usemi k.m. Aziza.

⇒ Mtamaaduni kama vile Salma na mamake msimulizi ambaye anamyependekezea mke.

⇒ Mwacha mila kama vile Fedhele anayevaa kanzu hadi mapajani.

⇒ Hana ubaguzi kama vile Aziza hambagui muuza madafu.

**Ubaguzi**

⇒ Msimulizi anakataa kuoa wanawake walioelimika kwa kuwachukulia hawana maadili na hawafuati utamaaduni. Kinaya ni kwamba amuoa mke aliye mtamaaduni.

⇒ Hataki muuza madafu aingie nyumbani kwake kwa kuwa ni duni.

**Ubwana**

⇒ Aziza hapendi ubwana.

⇒ Mapanya ni mtumishi na anafanya kazi ya kuosha nguo na vyombo.

**Busara/hekima**

⇒ Msimulizi anamjibu mkewe kwa upole na hivyo kuzuia mzozo kuwa mbaya zaidi.

**Bidii**

⇒ Muuza madafu ana bidii kwa kujiajiri mwenyewe badala ya kutegemea kuajiriwa.

**Ubahili**

⇒ Aziza anaonelea ni ubadhirifu mtu kutoa pesa zake nyingi anunue kiatu kisha akikanyagishe kinyaa na kinyesi majiani.

**Ujinga**

⇒ Aziza hana elimu na hajui athari ya kwenda msalani bila viatu.

**Matumizi ya lugha**

**Nidaha**

⇒ Ngnhngnh!-msimulizi akidharau Fedhele.

⇒ Barabara! Si watu kama vile ninyi?-Aziza kuudhika kwa msimulizi kudharau uchomaji na uuzaji mihogo kama kazi.

⇒ Lo! Mimi nikachome mihogo niuze?-msimulizi kushangaa kwa kupendekezewa na mkewe ajiajiri kazi kama ya uchomaji mihogo.

**Taharuki**

⇒ Kwa nini Aziza anamtazama msimulizi bila kumzungumzia?

⇒ Msimulizi alimpa aziza talaka?

⇒ Msimulizi alimwoa seluwa?

⇒ Msimulizi alitilia maanani mafundisho ya Aziza na kuanza kufanya kazi?

⇒ Aziza aliolewa na muuza madafu?

**Mbinu rejeshi**

⇒ Msimulizi kuwaza jinsi alivyomkuta Fedhele Salim Saateni saa mbili usiku kavaa kanzu mpaka mapajani, kafuatana na shoga yake na wanamtia kijana mwanamume katikati yao.

⇒ Anatufahamisha kuna siku wakati wa alasiri Seluwa alienda kuwatembelea yeye msimulizi na mkewe.

**Tashbihi**

⇒ Uko chini ya wazee wako kama mtoto anayenyonya-Aziza kwa msimulizi.

⇒ Ngozi yake ilivyokacha utadhani msasa-ngozi ya aziza kuwa ngumu kwa kazi za mikono za shambani.

**Takriri**

⇒ Muuza madafu amevaa kanzu mararu mararu.

⇒ Hebu! Hebu! Aziza akimnyamazisha Seluwa ahakikishe ni sauti ya muuza madafu amesikia.

⇒ Dafu! Dafu! –Sauti ya muuza madafu kama alivyoisikia msimulizi.

⇒ Najua wewe una fikra namna na namna-Msimulizi akimwambia Aziza.

**Balagha**

⇒ Mangapi umeng'olewa?-Aziza kuonyesha uduni wa mbinu za sasa za kutunzia meno

anazotumia msimulizi.
- ⇒ Sijui mimi nilikuwa narudi kutoka wapi vile?-wakati msimulizi alimuona fedhele usiku. Kinaya ni kuwa yeye pia alikuwa anatembea usiku na kachelewa kurudi nyumbani.
- ⇒ Kitu kilichokufa kina uzima gani wa kukuhami wewe?-Aziza akidharau kiatu.
- ⇒ Vipi mtu atafute kazi asipate?-Aziza kuonyesha mtu hawezi kukosa kazi hata kama ni ya kujiajiri.
- ⇒ Basi wewe ndiye mume wa kunioa mie we?-Aziza hamchukui msimulizi kuwa mumewe kwa kukosa kazi.

**Methali**
- ⇒ Kwenye nchi ya vipofu, mwenye jicho moja atakuwa mfalme.
- ⇒ Kila mtu na kazi yake.-msimulizi kuonyesha hawezi kufanya kazi za mikono.

**Nahau**
- ⇒ Nimvumbike mwenyewe mpaka aive-amuoe mwanamke amstaarabishe.
- ⇒ Kupatia mguu-Aziza hajawahi kufika mjini.
- ⇒ Tulikwenda sare kwa kupimana-msimuliz na Aziza kuwa sawa.
- ⇒ Kuwa na kidomo-hakumpenda salma kwa kusema maneno ya watu au kujibizana-kinaya ni kuwa aliyemwoa (aziza) anajibizana naye.
- ⇒ Nikawaweka kando-msimulizi kukataa kuwaoa wanawake aliochaguliwa eti hawana maadili.

**Taswira**
- ⇒ Fedhele salim kuvaa kanzu mpaka mapajani.-kuonyesha uigaji wa utamaaduni wa kigeni.
- ⇒ Salma Fadhil kujifunika uso na kujiremba marangi ya mAshavu na midomo-kuonyesha utamaaduni. Kinaya ni kuwa msimulizi anakataa utamaaduni ilhali yeye anaufuata kama vile kuchaguliwa mke na anaishia kuoa Aziza aliye mtamaaduni.
- ⇒ Alinionyesha viganja vyake nikaona namna ngozi yake ilivyokacha utadhani msasa.

**Chuku**
- ⇒ Hana kazi ya kumshughulisha labda kujikuna tu anapowashwa-mke wa msimulizi katu hakuwa na kazi yoyote, hakuwa na kazi wala basi.
- ⇒ Chukua mwiba unishindilie nyayoni mwangu utazame kama hautavunjika kabla ya kunichoma-Aziza kuonyesha jinsi miguu yake ilivyo madhubuti na haihitaji ulinzi wa viatu.
- ⇒ Alinionyesha viganja vyake nikaona namna ngozi yake ilivyokacha utadhani msasa.

**Kinaya**
- ⇒ Anwani mke wangu ni kinaya kwa vile mke aliyemtaka siye aliyempata. Alipata mwenye sifa zile alizozikataa kama vile utamaaduni, uhuru, mwenye usemi, n.k.
- ⇒ Kudhani mwanamke ndiye anastahili kuelekezwa (Niliona ni wakati wangu kumsoma Aziza ili nipate kumsomesha.) ilhali ndiye anahitaji kuelekezwa.
- ⇒ Kudhani Aziza kwa kutoka shambani, lazima awe mwepesi, msikivu na mwelekevu.
- ⇒ Kudhani Aziza angempenda kwa utajiri na angeridhika na maisha ya mjini ya kitajiri na starehe.
- ⇒ Kukataa salma kwa kuwa mtamaaduni na kuishia kuoa Aziza aliye mtamaaduni pia.
- ⇒ Kukataa kumwoa seluwa kwa kidomo chake na kuishia kuoa Aziza anayejibizana naye.
- ⇒ Kumkashifu Fedhele kwa kutembea usiku ilhali hata yeye alikuwa akitembea usiku.
- ⇒ Mtu ambaye amesoma na anayetoka katika familia tajiri kumwoa mwanamke ambaye hajasoma na anayetoka katika familia maskini.
- ⇒ Kuoa mwanamke wa shambani ambaye hajasoma na kutarajia asiwe mtamaaduni.

**Tabaini**
- ⇒ Aziza alikuwa daima akinitazama kwa kunichuja tena si mara moja wala si mbili.
- ⇒ Mimi sioni raha kulishwa na mtu ajinabi si baba yangu wala si mume wangu-Aziza hapendi utegemezi.

**Tashhisi**
- ⇒ Jawabu lake mtoto yule lilinizungusha kichwa darmadaru-majibu ya Aziza kumshangaza msimulizi.

**Utohozi**
- ⇒ Shilingi mbili-msimilizi alizompa Aziza akanunue madafu.
- ⇒ Burashi-ya kusugulia meno.
- ⇒ Plastiki iliyotengeneza kifurushi Aziza alikoweka mswaki na unga.

**Kejeli**
- ⇒ Nitapata mume wangu au gumegume tu?-Aziza akimdharau msimulizi kwa kuona hastahili kuwa mume wake.
- ⇒ Pesa mbili nobe zinakushinda kuzivumbua mpaka upewe?
- ⇒ Lazima tupokee kibivu maadamu mume wangu havumbui kibichi?
- ⇒ Kitu kilichokufa kina uzima gani wa kukuhami wewe?-kiatu
- ⇒ Kwa nini nichukue manyoya ya nguruwe nitie kinywani mwangu?-akidharau burashi ya kusugulia meno.

**Tanakali**

⇒ Aliondoka nyatunyatu akaenda zake ji-ji-Aziza akienda kuchukua vifaa vyake vya kusugulia meno.

**Sitiari**

⇒ Aziza kuita mswaki manyoya ya nguruwe.
⇒ Kukiita kiatu ngozi ya ngombe aliyekufa.
⇒ Pia kusema Kazi ndiyo maisha bora.
⇒ Kusema muuza madafu ni binadamu kamili.

# 2.Samaki wa Nchi za Joto

⇒ Anwani ni ya kiistiari
⇒ Kumaanisha unyonyaji au kitu unachokitumia kujifaidi.
⇒ Kuna samaki halisi wa nchi za joto ambao Peter anafanya bishara ya kuwauza nje ya nchi.
⇒ Serikali ya kikoloni kuleta samaki wa aina ya sangara walioangamiza samaki asilia katika maziwa.
⇒ Christine ni samaki kwa kutumiwa na Peter kutosheleza uchu wake. Pia daktari anamtoa mimba ili apate pesa.
⇒ Zac pia ni Samaki kwani Anamfahamu Peter kupitia Zac
⇒ Wavuvi ni samaki kwa vile Peter anawanunulia samaki kwa bei ya chini(kuwapunja) kAsha anawauza na kupata faida kubwa.
⇒ Watu weusi ni samaki kwa vile wanapenda pesa na pesa ni chambo chao.
⇒ Jagtit na Sunja kuibia nchi ya Uganda mapato ya ubadilishaji sarafu.
⇒ Sunja kumlaghai Jagtit kwa kumpa noti ya dola 100 bandia.
⇒ Zac na wengine wanaofanya kazi katika kampuni ya Peter ni Samaki kwani wanatumiwa naye katika biashara yake na faida kubwa ni yake.
⇒ Deogracious pia ni samaki kwani anafanya kazi ya utumishi wa nyumbani kwa Peter.
⇒ Nchi ni samaki kwani Peter anaiibia raslimali ya samaki na wahindi kama vile Sunjal na Jagtit wanaiibia pesa kwa kufanya biashara ya dola ya kimagendo.
⇒ Makahaba wanaotafutwa na wazungu huko ‘half London’ pia ni aina ya samaki kwani chambo chao ni pesa.

**Maudhui**

**Mapenzi nje ya ndoa/vyuoni/shuleni na athari zake**

⇒ Christine ni mwanafunzi wa shahada ya Sosholojia katika chuo cha Makerere. Aliye na tamaaa ya mpenzi wa kiume.
⇒ Tamaa yake inasadifiana na kutokea mzungu Peter anayemfahamu kupitia Zac.
⇒ Mwandishi anataka kuonyesha jinsi wasichana vyuoni wanavyojihusisha na mapenzi na watu walio na umri unaozidi wao ili wapate pesa (ushuga dadi).
⇒ Anaonyesha ukosefu wa uwajibikaji kwa vile Christine anapopata mimba anaamua kuitungua.
⇒ Anataka kuonyesha jinsi vijana wasivyochukulia maisha yao kwa umakini na tahadhari na hivyo kuishia kuyaharibu.
⇒ Jinsi watu wanavyojiingiza katika mapenzi ya kupitisha muda kama vile Peter na Christine hawakuwa na lengo la kuoana.

**Uzinifu**

⇒ Peter na Christine ni wazinifu kwa kufanya mapenzi ilhali hawajaoana.
⇒ Tunafahamishwa huko ‘half London’ kuna wazungu wengine wanatafuta makahaba (ukahaba).

**Uwajibikaji**

⇒ Peter hana uwajibikaji katika mapenzi kwani hamkingi Christine asipate mimba.
⇒ Hata hivyo Peter anawajibika katika kazi yake kwani halewi akiwa kazini.
⇒ Christine hawajibiki kwani hakubali mimba kama tokeo la vitendo vyake vya utovu wa uadilifu na kuilea bali anaamua kuiavya.
⇒ Zac anawajibika kwa vile anamfahamisha Christine kuwa Peter ana wasichana wengine.
⇒ Deogracius hawajibiki kwa vile hamfahamishi Christine kuhusu Peter ili amwambae.
⇒ Miriam na Margaret hawawajibiki kwani Christine alipowaeleza nia ya kutoa mimba hakuna aliyemzuia au kumshauri dhidi ya kufanya hivyo.

**Ukoloni**

**Mkongwe**

⇒ Serikali ya kikoloni kuleta samaki wa aina ya sangara walioangamiza samaki asilia.

**Ukoloni mamboleo**

⇒ Peter kupunja wavuvi kwa kuwanunulia samaki kwa bei ya chini(unyonyaji).
⇒ Peter kuibia nchi raslimali asili ya samaki.
⇒ Peter kuamrisha wafanyakazi wake kama mnyapara na akipaaza sauti ya juu.
⇒ Huko ‘Sailing Club’ kuna mahali pa wazungu na pa Waafrika.
⇒ Jagtit na Patel kufanya biashara ya magendo ya kuuza dola na hivyo kuibia nchi mapato ambayo ingepatika kutokana na ubadilishaji halali wa dola.

- ⇒ Huko Sailing Club ni mahali pa wazungu kwani ada ya juu ya kiingilio iliwafanya watu weusi kutopamudu.

**Ukosefu wa ajira**

- ⇒ Christine kusema mtu angepata kazi ya kiserikali kwa kubahatika.

**Madhila ya wafanyakazi**

- ⇒ Kuamrishwa-Peter Kuamrisha wafanyikazi wake kama mnyapara.
- ⇒ Kufanyia kazi katika mazingira duni-ofisi kuukuu za kikoloni.

⇒ Wavuvi wanaofanya kazi za mikono wana dhila la kupunjwa na wanaowanunulia wanaowanunulia samaki wao kwa mfano Peter.

**Athari ya kumtelekeza mungu/dini**

- ⇒ Christine alikuwa mkristo aliyeokoka lakini aliasi imani yake.
- ⇒ Hata dadake Dorothy alikuwa ameokoka lakini alikuwa mnafiki kwani alikuwa anajitia uongofu au anajificha chini ya kivuli cha dini.
- ⇒ Kujitia uongofu huko kukamchochea Christine kuendelea na mapenzi na Peter.
- ⇒ Christine kwa kuacha wokovu alitumbukia katika uzinifu na matokeo ni kutunga mimba na kuitungua.
- ⇒ Kuavya mimba kunamwathiri kisaikolojia kwa kuhisi amekosea Mungu na kuishi na woga wa madhara ambayo angepata kutokana na uavyaji mimba huo.

**Utabaka**

- ⇒ Peter ni wa tabaka la juu akiwa Uganda ilhali kwao Uingereza ni wa la chini la Cockney.
- ⇒ Deogracius, Zac na wengine ni wa tabaka la chini.
- ⇒ Huko Sailing Club ni mahali pa wazungu kwani ada ya juu ya kiingilio iliwafanya watu weusi kutopamudu.
- ⇒ Watu wa tabaka la juu kama Peter wanaishi katika mitaa ya kifahari kama vile wa 'Tankhill'.

**Tamaa**

- ⇒ Peter kununua dola kimagendo ili aokoe pesa ambazo angalinunulia dola halali katika benki.
- ⇒ Peter kupunja wavuvi ili ajipatie faida kubwa.
- ⇒ Peter ana tamaaa ya wanawake. Ana wengine mbali na Christine.
- ⇒ Peter ana tamaaa ya anasa kama vile zinaa, likizo Nairobi, ulevi, kula nyama choma na kunywa mvinyo na kutafuta makahaba.
- ⇒ Christine ana tamaaa ya mpenzi wa kiume.
- ⇒ Zac na wafanyakazi wengine wana tamaaa ya pesa ndio maana wanamfanyi Peter Kazi licha ya kudhalilishwa naye ka kuamrishwa kama mnyapara.
- ⇒ Jagtit na Sunja wana tamaaa ya pesa na ndiyo sababu ya kuuza dola za kimagendo.
- ⇒ Madaktari wana tamaa ya pesa na wanamtoa Christine mimba ili wazipate.
- ⇒ Ami nana tamaa ya uongozi na ndiyo sababu ya kutaka kuangamiza maprofesa wanaopinga uongozi wake dhalimu.
- ⇒ Christine anasema vijana wengine wana tamaa ya kuwa watu wakubwa anayoiita ndoto za kiwenda wazimu.

**Umaskini**

- ⇒ Zac kulazimika kufanya kazi katika kampuni ya Peter akisoma.
- ⇒ Deogracius anafanya kazi duni ya utumishi kwa Peter.

**Uongozi mbaya**

- ⇒ Iddi Amin kufanya jaribio la kuangamiza maprofesa jambo lililosababisha wao kukimbilia uhamishoni.

**Heshima**

- ⇒ Zac kuinuka na kumkaribisha Peter kiti alichokuwa anakalia.

**Ushauri**

- ⇒ Zac kumshauri Christine kuwa Peter ana wasichana wengine lakini hakutilia maanani ushauri wake (mapuuza).
- ⇒ Dorothy kumshauri Christine kuwa aliota wazungu wakimpa sumu lakini hakushaurika.
- ⇒ Margaret na Miriam hawamshauri Christine dhidi ya kuavya mimba na hivyo wanapuuza wajibu wao mkubwa wa kumhifadhi ndugu.

**Uavyaji wa mimba na athari zake/ukatili**

- ⇒ Athari za kisaikolojia kuhisi nafsi ikimsuta.
- ⇒ Kuwa tasa.
- ⇒ Kuwa muuaji.
- ⇒ Kumkosea Mungu.
- ⇒ Kufa.

**Matumizi mabaya ya taaluma**

- ⇒ Daktari kumtoa Christine mimba ili apate pesa badala ya kumpa ushauri mwema.

**Kasumba**

- ⇒ Zac kutamaani kuwa mmarekani mweusi kwa kupenda kuzungumza sana kama mmarekani mweusi-'Hey man'.
- ⇒ Kuheshimu wazungu kwa kuchukulia wazungu wote kama wa tabaka la juu ilhali kwao hawaheshimiwi kwa kuwa wa tabaka la chini.
- ⇒ Watu wa rangi moja kuaminiana kwa mfano Jagtit kumwamini Mhindi mwenzake Sunja Patel ilhali anaishia kumtapeli.

**Umuhimu wa kuwa makini**

*©Bw. P.K Mwirigi (mwongozo wa Damu Nyeusi)*

⇒ Peter ni makini kwa kuzikagua dola hadi kupata kuna noti moja bandia.
⇒ Jagtit hakuwa makini akipewa noti za dola na Patel ndipo akatapeliwa.

**Bidii**
⇒ Zac anafanya kazi katika kampuni ya Peter akiwa angali anasoma.
⇒ Peter ana bidii katika kazi yake na hatumii muda wa kazi kujistarehesha.

**Anasa/starehe**
⇒ Ulevi k.m. uvutaji sigara, kunywa pombe, uzinzi, Peter kwenda likizo Nairobi kustarehe baada ya biashara kunoga, Christine kujipumbaza kwa mvinyo, Margaret kulewa n.k.

**Utovu wa Uaminifu**
⇒ Peter ana wasichana wengine mbali na Christine.
⇒ Christine na dadake Dorothy si waaminifu kwa Mungu.

**Ulevi na athari zake**
⇒ Kusababisha Christine kuwa mzinifu.
⇒ Uzinifu kusababisha mimba isiyotakikana.
⇒ Unusu kaputi kutofanya kazi Christine akitolewa mimba.

**Upyaro**
⇒ Peter kumita Jagtit mwanaharamu anapotaka kuchukua vipande vya noti bandia.

**Unafiki**
⇒ Deogracius hamwambii kuwa Peter Peter ana wapenzi wengi.
⇒ Dorothy kuwa na wokovu bandia na anatumia dini kama kivuli (ulokole).
⇒ Peter kuwaonyesha Zac na Christine urafiki kumbe ataka kumtumia Christine.
⇒ Miriam ni rafiki mnafiki kwani hamshauri Christine dhidi ya kuavya mimba.

**Uhalifu**
⇒ Jagtit kumuuzia Peter dola kimagendo ilhali lilipaswa kufanywa na benki kuu.
⇒ Sunja kumpatia Jagtit pesa bandia.
⇒ Utoaji wanawake mamba.

**Taasubi ya kiume/udunishaji wa wanawake**
⇒ Peter kutumia wanawake kama vyombo vya kujiburudisha.
⇒ Wazungu kuwatumia makahaba kujistarehesha.

**Utamaushi/ujidunishaji**
⇒ Christine anajiingiza katika mapenzi kwa ili kujipumbaza au kujidanganya kuwa mtu mwingine au kuwa dubwAsha tu- ujidunishaji.
⇒ Anasema akiwa na na shahada angekuwa kama ng'ombe wa kizungu kwa vile hakuna ajira na ikipatikana mazingira ya kazi ni mabaya na mishahara ni duni.
⇒ Vijana hujiingiza katika myenendo isiyofaa kwa kupoteza matumaini ya maisha ya kesho.

**Uingiliaji wa mambo ya wengine**
⇒ Watu kumkodolea macho kwa kubusiwa na Peter shavuni.
⇒ Wakasema 'Hawa Malaya hawana aibu hata chembe'.
⇒ Atakuambukiza ukimwi.
⇒ Ona alivyokondeana.

**Ubwana**
⇒ Deogracius ni mtumishi wa Peter.
⇒ Wafanyakazi wa Peter anaowaamrisha kama mnyapara.

**Ukengeushi**
⇒ Miriam na Christine kunywa pombe.
⇒ Miriam kuvuta sigara.
⇒ Mapenzi nje ya ndoa.
⇒ Kutembea kwa wanaume.
⇒ Uavyaji mamba.
⇒ Christine kuacha imani yake na Dorothy kuwa mlokole.

**Ukweli**
⇒ Zac kuonya Christine Peter ana wanawake wengi.

**Matumizi ya lugha**

**Tashhisi**
⇒ Nilivaa tabasamu niliyowahifadhia wanaume, tabasamu ya geresha-Christine kwa Peter.
⇒ Nilijaribu kumjibu lakini sauti ilinikwama kooni. Ukatokea mnong'ono.
⇒ Aibu ilinivaa-Christine akitoka kwa Zac baada ya kukutana na Peter kwa kushindwa kumjibu Peter au kusema haja ya moyo wake.
⇒ Nilikuwa nikiwangwa na kichwa changu kutokana na hedhi.
⇒ Springi za kitanda kulalamikia uzito wake wa ziada-kutoa kelele Peter alipokalia na kuzidisha uzito.
⇒ Mvinyo ulikuwa umenipa ujasiri fulani-Christine kutojishughulisha na Peter.
⇒ Macho yake kila mara yalinihukumu-ya Deogracius.
⇒ Wacha ukimwi uwateketeze-uwaangamize-wakati amemsindikiza Peter akielekea Nairobi.
⇒ Kutokana na mpito wa wakati, nywele za Peter kuwa zinabadilika rangi pengine kutokana na shinikizo la biashara ya nchi za nje ya samaki.
⇒ Nikaachwa nikiadhibiwa na mikondoo ya macho ya watu-baada ya kubusiwa shavuni na Peter.
⇒ Jua liliendelea kuadhibu kila kiumbe –kuwaka

vikali Christine akiwa katika matatu.

**Taswira**

⇒ Deogracius amepinda mgongo kwa umri na mwenye miguu ya matege.

⇒ Kwa Peter, michoro ya kisana ilitundikwa ukutani, makabati ya vioo yaliyosheheni vinywaji vya aina aina na vyombo vya kichina-utajiri.

⇒ Chumba cha Zac kina kuta zilizobambuka rangi, balbu iliyotoa mwangaza hafifu, picha kubwa ya Bob Marley iliyorarukararuka, vitabu vikuukuu viwili vya 'Penguin Classics', kitanda chake kimetandikwa blanketi ya rangi ya kahawia.

⇒ Zac kufungua kikabati kidogo cheusi akatoa sahani mbili nyekundu za plastiki zilizoonyesha kuwa na mafutamafuta, kikombe cha kijani kibichi cha plastiki na glasi iliyokuwa na mavumbi.

⇒ Nikatabasamu nikitaka aone meno yangu yenye weupe wa maziwa.

⇒ Noti za dola za kijani kibichi.

⇒ Wajihi wa Peter ulikuwa wa wekundu usiokoza na wala sio weupe usiotakata. Nywele zake tu ndizo zilikuwa nyeupe

⇒ Tankhill, makasri ya mabalozi yalizungushwa kuta za mawe, juu ya kuta hizo kumechomekwa vigae vya chupa. Kuna mabwawa ya kuogelea na walinzi wa kulipwa-kuonyesha utabaka.

⇒ Peter, akiwa na bombo (kaptula) aliyoipenda sana, alionekana kama mvulana wa miaka 14.

⇒ Alikuwa na maungo mviringo ya ujana, mwili laini kama wa mwanamke na miguu iliyobonyea na iliyopuuka.

⇒ Miriam rafiki yake Christine ni Mtutsi aliyekuwa na wembamba waliopendelea wazungu na macho ya vikombe.

**Mdokezo**

⇒ Mwiba wa kujidunga… chochote kingetokea akitolewa mimba na asingemlilia au kumlaumu yeyote.

⇒ Fikra zilinipaa kuhusu matokeo ya uovu huu; kuwa tasa… labda kuwa muuaji… ahh… kumkosea Mungu… pengine hata kufa-madhara ya uavyaji mimba.

⇒ Lakini ni…nina jambo nataka kukwambia-Christine -Peter anapomwambia hana nafasi ya kumuona wakati wafanya kazi wanapakia mizigo.

⇒ Angalia hapa… Peter akimwabia jagtit ahakikishe noti ni bandia.

**Methali**

⇒ Mwiba wa kujidunga…

⇒ Palikuwa na kimya chenye mshindo-baada ya Zac kuwaacha na Peter-walinyamaziana.

**Taharuki**

⇒ Mwisho wa Christine na Peter ulikuwaje?

⇒ Baada ya kuavya mimba, afya ya Christine ilikuwaje?

⇒ Jagtit alimchukulia hatua gani mhindi mwenzake Sunja kwa kumpa noti ya dola 100 bandia?

**Ujinga**

⇒ Jagtit kutapeliwa na Sunja kwa kutokagua dola kwa kumwamini eti kwa vile ni wa asili yake hawezi kumlaghai.

⇒ ,Christine kuwa na uhusiano wa kimapenzi na mtu asiyemfahamu vyema.

⇒ Kufanya mapenzi bila kinga.

⇒ Kutofahamu tama mbele mauti nyuma.

⇒ Kutoshaurika.

⇒ Kuacha Mungu akijua amwachaye hawezi kuwa na maisha mazuri.

⇒ Kuavya mimba akijua madhara yake na kuua mtoto ilhali hana hata mmoja.

**Balagha**

⇒ Mbona tusijipatie kinywaji-Zac.

⇒ Ningemwambiaje Peter akinipigia simu?-Baada ya kuavya mimba.

⇒ Mimi? Kwa nini?- Christine Zac anapomwambia Peter alitaka wamtembelee Tankhill-kujifanya hataki ilhali anataka.

⇒ Je, Ni kweli Peter alinitaka?-Christine. kujiuliza kimoyomoyo.

⇒ Kumbe alikuwa mzungu wa tabaka la chini?

**Nahau**

⇒ Tunapiga gumzo-Peter kuingia na kukuta Christine na Zac wakiongea.

⇒ Kufyata mkia-Christine-Peter alistahili kunyamaza kwa vile alikuwa anaibia nchi samaki.

⇒ Sikutaka kukitia kitumbua cha uhusiano wetu na Peter mchanga-kuharibu mapenzi yao licha yake kuwa na wasichana wengine.

⇒ Kupiga funda kubwa-Christine kujaza kinywaji kwa mara moja baada ya kushindwa kumjibu Peter.

⇒ Nimeavya mimba-nimetoa kijusi tumboni.

⇒ Niligundua ulikuwa Mja mzito-Peter.

⇒ Mwili haukufa ganzi-haukupoteza hisi baada ya sindano ya nusu kaputi-athari ya ulevi.

⇒ Alimpasulia mbarika-Peter kumpa Jagtit habari mbaya kuwa noti ni bandia.

**Kinaya**

⇒ Christine kujivuta kidogo mbali na Zac ilhali

anamtaka.

- ⇒ Wewe lazima u msichana mwerevu-Peter-ni kinyume.
- ⇒ Mimi? Kwa nini? Christine Zac anapomwambia Peter alitaka wamtembelee Tankhill-kujifanya hataki ilhali anataka.
- ⇒ Zac usiwe mpumbavu. Mimi sitakwenda-anataka kwenda.
- ⇒ Christine kusomea sosholojia ilhali mwenendo wake ni wa kukengeuka.
- ⇒ Kunyoosha mkono wake alioulegeza kimakusudi kumsalimu Peter-kama htaki ilhali anataka.
- ⇒ Sauti ya mchuuzi aliyepaaza sauti akimsihi awanunulie watoto wake peremende na kumwambia, "shangazi wakumbuke watoto na waonee huruma".-ukweli ni kuwa ametenda kitendo cha kikatili cha kuavya mimba.
- ⇒ Christine kuavya mimba ilhali hana mtoto mwingine.

**Utohozi**

- ⇒ Ofisi ya Peter
- ⇒ Maprofasa-wahadhiri wa chuo kikuu
- ⇒ Balbu-taa
- ⇒ Jenereta-kwa Peter-lililojiwAsha umeme ulipopotea
- ⇒ Wikendi
- ⇒ Shati-aliyovaa Peter akielekea Nairobi
- ⇒ Glasi
- ⇒ Sahani mbili nyekundu za plastiki
- ⇒ Springi za kitanda
- ⇒ Kozi-taaluma
- ⇒ Noti ya dola 100 yenye thamani ya shilingi 1,000,000

**Tashbihi**

- ⇒ Peter kumuuliza Christine anasomea kozi gani kama mjomba mkarimu anavyomuuliza mpwa wake.
- ⇒ Ulaini wa ngozi yake (peter) ulikuwa sawa na wangu.
- ⇒ Peter aliniongoza katika chumba chake cha kulala kama kwamba hilo lilikuwa jambo la kawaida.
- ⇒ Peter kuangalia noti bandia kama mwanasayansi aliyekuwa akifanya uchunguzi maabarani-umakini.
- ⇒ Uhusiano wetu niliuona kama kitendo cha watoto kwenda shuleni-kulazimika/kutokuwa na budi.
- ⇒ Mhindi alimtumbulia macho kama kwamba alikuwa mzuka-Peter akikagua noti bandia.
- ⇒ Baada ya kujihisi salama niliingiwa na wazo la kuwa debe bovu-kumfahamisha Peter hali yake ya hedhi.
- ⇒ Nilitembea barabarani kama mtembea usingizini hadi katika kituo cha matatu-akitoka kwa Peter ofisini baada ya kumwambia aliavya mimba.
- ⇒ Nikiwa na shahada ningekuwa kama ng'ombe wa kizungu-utamaaushi-hata akisoma, hakuna kazi ,mishahara duni, mazingira mabaya-ofisi kuukuu zilizojengwa wakati wa ukoloni.
- ⇒ Umati ulipasua kicheko nilichokisikia kama radi.

**Mbinu rejeshi**

- ⇒ Christine alikuwa ameokoka wakati mmoja
- ⇒ Kisa cha Jagtit alichoshuhudia Christine alipompa Peter noto ya dola banda aliyokuwa amepewa na mhindi mwenzake Sunja Patel.
- ⇒ Christine kueleza jinsi urafiki wao na Peter ulivyoanza kupitia Zac anayefanya kazi katika kampuni yake.
- ⇒ Zac kueleza Christine jinsi Peter alivyoenda 'Sailing Club' na msichana mwingine.
- ⇒ Kufahamishwa kuwa siku nyingi za Ijumaa jioni, Christine alikuwa anaondoka chuoni na kwenda kumtembelea Peter.

**Jazanda/ Sitiari**

- ⇒ Anwani Samaki wan chi za Joto ni Jazanda.
- ⇒ Samaki waliowala wale asili ni ukoloni mamboleo.
- ⇒ Ndoto ya Dorothy kuhusu Christine ambapo aliota siku moja Christine alikuwa akipewa <u>sumu</u> na wazungu-akiharibiwa maisha.
- ⇒ Huu ulikuwa msalaba wangu-mimba ni wajibu Christine pekee kwani hawakupanga na Peter kupata mtoto.

**Sadfa**

- ⇒ Kukutana kwa Christine na Peter kupitia Zac wanayesoma naye Makerere na anayefanya kazi katika kampuni ya Peter.

⇒ Christine kuwa kwa Peter kunasadifiana na Jagtit kumtembelea Peter kumuuzia dola.

**Uzungumzi nafsia**

⇒ Wewe baradhuli, kwa nini hukusema jambo lolote la maana- Christine akitoka kwa Zac akijisuta kwa kutochukua fursa kuanzisha urafiki na Peter.

⇒ Nikweli Peter alinitaka?-Christine kujiuliza kimoyomoyo.

⇒ Kwani Zac alifikiria sikumjua Peter vyema?-anapoambiwa walienda sailing club na msichana mwingine.

**Kuchanganya ndimi**

- ⇒ 'Penguin Classics'-vitabu vilivyokuwa juu ya dawati ya Zac.

⇒ 'Hey man'-kasumba ya Zac kuiga Waafrika weusi.
⇒ 'Half London'-wazungu wanakotafuta makahaba.

**Takriri**

⇒ Najihisi mlevi, mlevi saana-na-Miriam.
⇒ Hapana, hapana haiwezi kuwa bandia-jagtit kwa peter -kutoamini noti ni bandia.

**Kicheko/tashtiti**

⇒ Christine kucheka akimwambia Peter kuhusu ndoto ya Dorothy.
⇒ Peter kucheka anapoambiwa ndoto ya Dorothy na Christine.
⇒ Umati ulipasua kicheko nilichokisikia kama radi.

**Chuku**

⇒ Jagtit alipigwa na butwaa asiweze kuhoji kitendo cha Peter-kurarua noto bandia.
⇒ Umati ulipasua kicheko nilichokisikia kama radi-baada ya kumsikia kijana aliyempaazia Peter Sauti kuwa angeambukizwa ukimwi na Christine.
⇒ Kuwepo Entebbe Sailing Club kungemfanya awe mweusi zaidi-wengi ni wazungu.

**Kejeli**

⇒ Kicheko ni kejeli kwa mtu kwa kutenda kitendo cha kijinga.
⇒ Christine kusema akiwa na shahada angekuwa kama ng'ombe wa kizungu-elimu isingeboresha maisha yake.
⇒ Christine anasikia sauti ya kejeli katika kicheko cha Peter anapomwambia ndoto kikisema watu weusi ni wajinga na washirikina wakubwa.
⇒ Kijana anayempaazia Peter sauti akimkejeli Christine akisema kuwa angemwambukiza akimwi na alivyokondeana.

# 3.Damu Nyeusi

**Maudhui**

**Kubaguliwa kwa watu weusi katika nchi ya Marekani**

- Kuachwa na mabasi ya abiria yanayoendeshwa na wazungu katika kituo wanapokuwa peke yao kwa kufikiriwa ni majambazi.
- Kukamatwa kwa makosa ambayo watu weupe hawakamatiwi kama vile kuvuka barabara taa nyekundu zikiwaka.
- Adhabu kali kwa makosa wanayofanya-alitozwa faini ya dola 200 au miezi sita gerezani kwa kosa la kutofunga zipu.
- Mkahawani, wanatazamwa kwa dharau na wateja na wahudumu.
- Kufuatwafuatwa na walinzi madukani kwa kushukiwa wataiba.
- Kuonewa vyuoni na wahadhiri wanaotoa alama kwa kupendelea watu weupe na kukandamiza wanafunzi weusi-hawapati shahada wanan'ang'ania kula kalenda au wanakaa muda mrefu bila kuhitimu.
- Huko marekani watu weusi ndio wengi magerezani-jela imeundiwa mtu mweusi.c
- Kutazamwa kwa kudharauliwa na wahadhiri weupe.
- Kuulizwa maswali ya dharau na wahadhiri wazungu na wanafunzi weupe.
- Mikahawani kumtazamwa kwa chuki na wateja na wahudumu.
- Kutendewa vitendo visivyo vya utu kama vile Fikirini aliposahau kufunga zipu, mama mzungu alimwitia polisi ilhali angemwambia tu afunge duka.

**Utovu wa utu wema**

⇒ Mama mzungu kumwitia Fikirini polisi badala ya tu kumwambia afunge zipu.

**Nafasi ya mwanamke**

⇒ Ni Kitega uchumi kama vile Fiona ni kahaba na anamuuliza Fikirini kama angependa wafanye mapenzi.
⇒ Ni mbaguzi kwa sababu mama mkahawani anamwitia polisi kwa kutofunga zipu kwa vile ni mweusi.
⇒ Hawana utu kwa vile Fiona anataka apigwe risasi hata anataka kumkata uume (mrija).

**Ujinga**

⇒ Baada ya kubaguliwa na kudhalilishwa anaamua kujitoa ukiwa wake kwa kuwa karibu na watu weusi ndugu zake waathiriwa wenzake.
⇒ Fikirini kumwamini Fiona na kumfuata ilhali hamjui wala hajamchunguza.

**Uzalendo**

⇒ Kwa kubaguliwa, Fikirini anaanza kujithamini na kupenda asili yake.
⇒ Anaomba muda umalizike arudi nyumbani.
⇒ Tunahimizwa kuthamini utu wetu/bara letu.
⇒ Nyumbani ni nyumbani ingawa pangoni.
⇒ Mtu asiyependwa na wengine sharti ajipende, ajienzi na ajionee fahari.

**Ulevi**

⇒ Fikirini anakumbuka jinsi walilewa waragi na chang'aa katika vitongoji duni vya Mathare.

**Elimu**

⇒ Fikirini ameenda marekani kusomea shahada ya uzamifu katika somo la kiingereza.

**Usaliti**

- ⇒ Mama mzungu kumsaliti Fikirini anapomwitia polisi kwa kusahau kufunga zipu.
- ⇒ Wamarekani weusi kusaliti Waafrika wenzao kwa hata wao kutenda vitendo vya kuwadunisha kama vile maswali ya kejeli kama Bob kumuuliza Fikirini kwa nini hakai huko kwao kwenye uchawi na washirikina.
- ⇒ Hata hawawasalamu watu wa asili yao.
- ⇒ Waafrika wamejisaliti kwa vitendo vyao viofu kama ujambazi na ndiposa wanabaguliwa na wazungu.
- ⇒ Wazungu wamewasaliti Waafrika kwa kuwabagua.
- ⇒ Fikirini amesaliti Afrika na Nchi yake kwa kwenda kusomea Marekani akiwa ameacha Vyuo huko.

**Huruma**

- ⇒ Bob anamkataza Fiona Kumkata Fikirini uume.
- ⇒ Hampigi risasi Fiona anapotaka afanye hivyo.
- ⇒ Anamrushia nguo ili asiende uchi.
- ⇒ Fiona ana huruma-ni katili.

**Ukatili**

- ⇒ Wa Fiona.
- ⇒ Waafrika kuendelezxa utamaduni wa kukeketa wanawake ili kupunguza tama ya zinaa.

**Matatizo yanayokumba bara la Afrika/mambo yasiyo ya uaminifu yanayohalalisha kubaguliwa kwa mtu mweusi**

- ⇒ Ujambazi/uporaji kama wa Bob na Fiona.
- ⇒ Kushindwa kupambana na umaskini-wanang'ang'ania mkono kufika kinywani.
- ⇒ Vita
- ⇒ Tamaaduni mbovu kwa mfano kukeketa wasichana.
- ⇒ Uchafu
- ⇒ Kasumba ya kudharau mtu wa ngozi yake na kuwaheshimu wazungu sana kwa kuwachukulia wote ni wa tabaka la juu.
- ⇒ Utovu wa maadili kama vile ujambazi na ukahaba unaoendelezwa na Fiona na Bob.
- ⇒ Kutojithamini kwa mfano Fikirini ameacha vyuo nchini mwao na Bob na Fiona wanaishi katika mazingira machafu.
- ⇒ Kushindwa kupambana na magonjwa.
- ⇒ Uchawi/ushirikina.

**Umaskini**

- ⇒ Watu wa Afrika kupigania mkono kufika kinywani na hivyo hawana wakati wa kufikiria kuhusu rangi.
- ⇒ Kuna kitongoji duni cha mathare huko Nairobi na Kibuye huko kampala.

**Kasumba**

- ⇒ Wamarekani weusi kukataa uAfrika.
- ⇒ Waafrika wakiwa uzunguni hawasalimu Waafrika wenzao.
- ⇒ Fikirini kutozwa faini kubwa na jaji mweusi.
- ⇒ Fikirini kuzungumza kama mmarekani mweusi ' Whets up men?'
- ⇒ Waafrika kuwaabudu watu weupe.-Fikirini kusema anAshangaa vile kwao wanavyowaabudu watu hao wasiowajali.

**Ukahaba**

- ⇒ Fiona ni kahaba na anamuuliza Fikirini 'Do you want a good time, hapa ukumbini patatufaa.

**Unyag'anyi/utapeli/ujambazi**

- ⇒ Fiona na Bob walimtapeli Fikirini dola 300.

**Uongo**

- ⇒ Fiona kusema Bob ni nduguye.
- ⇒ Fiona kudai Fikirini anataka kumbaka.
- ⇒ Fiona kusema ana gari-'Gari langu ni lile pale'.
- ⇒ Waingie nyumbani achukue ufunguo.

**Unafiki**

- ⇒ Fiona kumhakikishia Fikirini usalama wake.
- ⇒ Kumwambia ajihisi yuko kwake au kwao.
- ⇒ Kumwambia 'You guys are our brothers' anaposikia atoka Afrika.

**Ndoa**

- ⇒ Wamarekani hawajui kutunza ndoa.

**Heshima**

- ⇒ Fikirini kupita bila kumgusa Fiona akiingia kwake.

**Upyaro**

- ⇒ Bob kusema Waafrika ni wajinga na wenye ushirikina.
- ⇒ Kumwita Fikirini fala.

**kejeli**

- ⇒ Je, kule kwenu watu huvaa nguo au hutembea rabana?
- ⇒ Je mwaishi mitini kama tumbiri?
- ⇒ Mbona hambaki kwenu huko kwenye uchawi na ushirikina-Bob.
- ⇒ Huu weusi wenu unaozidi kiza unatokana na kuangukiwa na lami au kupigwa na mionzi ya jua?
- ⇒ Ni upi mji mkuu wa Afrika.
- ⇒ Mtu anaugua ukimwi malaria na polio na utapia mlo huko Afrika?
- ⇒ Mbona hamwachi kupigana nchini kwenu?
- ⇒ Nani anataka kuuona uchi wako?
- ⇒ *You*, wataka kumbaka dadangu kwa nini?
- ⇒ Nini kinawatoa Afrika kuja kutusumbua hapa marekani?-Bob-kasumba
- ⇒ Fala kabisa twawezaje sisi kuwa ndugu na

tumbiri kama nyie-Bob-kasumba.

⇒ Mbona hambaki kwenu huko kwenye uchawi na ushirikina wenu?-Bob-kasumba

**Balagha zaidi**

⇒ Mambo ya aibu kama haya unaweza kuwaelezea ndugu zako nyumbani?-kisa cha kutofunga zipu.

⇒ Sasa polisi gani angejua kiingereza kuliko mwanafunzi wa uzamifu katika somo la kiingereza katika chuo kikuu?

**Chuku**

⇒ Huu weusi wenu unaozidi kiza unatokana na kuangukiwa na lami au kupigwa na mionzi ya jua?

⇒ Mtu sharti avae safu ya maguo pamoja na viatu, viatu vizito kama vya wanajeshi wan chi kavu.-wingi wa baridi.

⇒ Hakuhisi mzizimo wa theluji iliyokuwa inaanguka kama matone ya mvua ya mawe.-anapoambiwa atoke kwa kina Fiona na Bob. Haja ni kunusuru maisha yake.

⇒ Jibaba la miraba mine-Bob.

⇒ Jimama lililofungAsha si haba-Fiona.

⇒ Kila kitu cheupe katika nchi hii,mtu mweusi apate wapi sauti na satua-kutilia mkazo ubaguzi wa Waafrika.

⇒ Alikuwa pandikizi la jimama-Fiona

⇒ Hata akilewa gongo,waragi au chang'aa kiasi cha bahari ya hindi hawezi sema kisa cha zipu kwa aibu.

⇒ Huu weusi wenu unaozidi kiza unatokana na kuangukiwa na lami au kuchomwa na mionzi ya jua?

⇒ Kijasho chembamba kikaanza kumtoka kipajini na kwapani-kusisitiza uoga Fikirini anapogusa mlango kwa Fiona na kukuta umekomelewa.

⇒ Akaumimina mkojo kwenye sakafu ya ukumbi kutokana na hofu-kwa kuonyeshwa mtutu wa bunduki na Bob.

**Takriri**

⇒ Mtu sharti avae safu ya maguo pamoja na <u>viatu</u>, <u>viatu</u> vizito kama vya wanajeshi wan chi kavu.-kusisitiza jinsi baridi ilivyo nyingi.

⇒ Alijotosa nje <u>tuputupu</u> kama alivyozaliwa-bila nguo akitoka kwa Fiona.

⇒ Tabasamu ilikutana na tabasamu-Fikirini akichekesha Fiona.

⇒ Fikirini kuzoa nguo na kukimbia <u>tuputupu</u> kama mtu aliyepagawa pepo mbaya.

Theluji kufunika kila ncha na kujenga mandhari nyeupe nyeupe.

**Tashbihi**

⇒ Mtu sharti avae safu ya maguo pamoja na viatu, viatu vizito <u>kama</u> vya wanajeshi wan chi kavu.

⇒ Mambo mengine yanakuwa <u>kama</u> ndoto au jinamizi-kisa cha mkahawani.

⇒ Akitetemeka kama majani ya mgomba kwenye dhoruba.

⇒ Fikirini kuzoa nguo na kukimbia <u>tuputupu</u> kama mtu aliyepagawa pepo mbaya.

⇒ Ananyapia nyapunyapu na kupepesuka <u>pepesupepesu</u> kama mlevi chakari.

⇒ Ananyapia nyapunyapu na kupepesuka pepesupepesu <u>kama</u> mlevi chakari-akielekea chuoni baada ya kuachwa na basi.

⇒ Fikirni alisihi akilia machozi kama mtoto mdogo -Fiona anaposema 'I say shoot him Bob'.

⇒ Theluji kufuniaka kila kitu kama blanketi la unga.

⇒ Hakuhisi mzizimo wa theluji iliyokuwa inaanguka kama matone ya mvua ya mawe.

**Taswira**

⇒ Mtu sharti avae safu ya maguo pamoja na viatu, viatu vizito kama vya wanajeshi wa nchi kavu.

⇒ Mikononi kafunika vitanga na vidole kwa glavu nyeusi.

⇒ Theluji kufunika kila ncha na kujenga mandhari nyeupe nyeupe.

⇒ Jimama lililofungAsha si haba-Fiona-mnene.

⇒ Jibaba la miraba mine lililokuwa limevaa miwani ya jua-Fiona.

⇒ Maguo machafu yametapakaa kiholela sakafuni, vumbi limetapakaa kwenye kochi.-uchafu kwa Fiona na Bob.

**Utohozi**

⇒ Glavu-za kuzuia baridi.

⇒ Dola-alitozwa faini ya dola 200 kwa kutofunga zipu na kuporwa dola 300.

⇒ Faini

⇒ Hana <u>makadi</u> yake mbalimbali-baada ya kuporwa.

**Kinaya**

⇒ Fikirini kushikwa kwa kutofunga zipu ilhali wanawake huko hawashikwi licha ya kutembea bila nguo.

⇒ Polisi kumuuliza kama anafahamu kiingereza ilhali anakifahamu hata kuliko wao kwani anakisomea.

⇒ Kusema jaji mweusi alikuwa na imani kwa kumtoza faini ya dola 200.

Nyani haoni kudule-kasoro

Kuchanganya ndimi

⇒ Sarafu kadha za <u>quarter</u>-robo kadha za dola.

⇒ How you doing?-Fiona.

⇒ Someone called to say you are exposing

yourself-polisi.
- ⇒ Am cool-Fikirini-kasumba.
- ⇒ Come fast this dude wants to rape me-uongo wa Fiona.
- ⇒ Do you speak English-polisi.
- ⇒ I say shoot him Bob-ukatili wa Fiona.
- ⇒ Get out of here-Bob akimfukuza Fikirini baada ya kumpora.

**Sitiari**
- ⇒ Kisiwa cheusi kwenye bahari ya weupe-Fikirini pekee ndiye mweusi darasani.

**Tashhisi**
- ⇒ Rangi mbili zinazokinzana na kufarakana –taswira ya Fikirini kuhusu vita vya watu weusi na weupe.
- ⇒ Wanawake wenu hawapendi nguo tena zimewachosha na kuwachusha.
- ⇒ Bado baridi inapenyeza na kuteketeza vyanda.

**Mbinu rejeshi**
- ⇒ Anavyotukumbusha jinsi alivyoepuka jela wakati alienda mkahawani baada ya kula akaingia msalani akasahau kufunga zipu.
- ⇒ Kukumbuka maneno ya Moi.
- ⇒ Kukumbuka siku walilewa waragi katika vitongoji duni-Kibuye-Kampala na Mathare-Nairobi.
- ⇒ Fikirini akilia anakumbuka kifo cha mamake akiwa katika shule ya upili.
- ⇒ Tunaarifiwa Fikirini mara mbili ametozwa faini na polisi.
- ⇒ Kukumbuka mara ya kwanza alipokwenda darasani jinsi yeye pekee alikuwa mweusi.

**Taharuki**
- ⇒ Fikirini alimaliza masomo yake au alikula kalenda?
- ⇒ Nini kinawafanya wamwangalie vibaya akitoka msalani?
- ⇒ Ilikuwaje alipofika chuoni bila vifaa hata kadi-vitambulisho?

**Nahau**
- ⇒ Kutia na kutoa kidogo-Kusitasita na kukataa anapoambiwa aingie na Fiona.
- ⇒ Funga duka-zipu.
- ⇒ Akachutama na kumwomba amwonee imani-amhurumie-Fiona anapopeleka kisu kwenye kinena cha Fikirini akitishia kumkata mrija.
- ⇒ Ajionee fahari-ajijivunie.
- ⇒ Alipopiga darubini nyuma alimwona mama mzungu kama hasidi-alipokumbuka.
- ⇒ Kula kalenda-kukaa miaka mingi bila kufuzu.
- ⇒ Fikirini amekaziwa macho vibaya-kuangaliwa vibaya kwa kutofunga zipu mkahawani.
- ⇒ Likija basi lingine na ambalo usukani wake umeshikwa na dereva mweupe mwenye mwoyo mweusi (mwoyo mbaya) yamkini mambo yatakuwa yale yale.
- ⇒ Maji yamezidi unga-baada ya kuambiwa na Fiona wawe na *good time*-ukahaba.

**Tanakuzi**
- ⇒ Likija basi lingine na ambalo usukani wake umeshikwa na dereva mweupe mwenye mwoyo mweusi yamkini mambo yatakuwa yale yale.
- ⇒ Anatamani arudi kwao na kufaidi utajiri wa umaskini wao ajitenge na umaskini wa utajiri wa marekani.
- ⇒ Faraja ya wazungu ni kuona ndugu zake weusi wananyanyasika katika mfumo unaomtweza mweusi na kumkweza mweupe

**Methali**
- ⇒ Nyumbani ni nyumbani ingawa pangoni-uzalendo.
- ⇒ Simba akikosa nyama hula nyasi-Fikirini kutopendelea chakula cha marekani na kulazimika kukila kwa kukosa aina nyingine.
- ⇒ Usipopendwa jipende-kuhimiza watu kujithamini.
- ⇒ Leo ni siku ya nyani kufa na ambapo miti yote huteleza-hakuna jambo lake linalofaulu.

**Kicheko**
- ⇒ Fikirini kucheka kauli ya Moi akidhani haina mashiko.

**Tabaini**
- ⇒ Si kuta, si majani, si matawi-kuonyesha taswira ya theluji kufunika kila mahali.

**Majazi**
- ⇒ Fikirini-kujisaili kufikiri zaidi kabla ya kwenda ng'ambo.

**Mdokezo**
- ⇒ Siku ya kufa, kifo cha aibu na nguo amevuliwa…
- ⇒ I say remove your clothes or else…

# 4.Glasi Ya Mwisho Makaburini
- ⇒ Hao marafiki kunywa pombe ya mwisho huko.
- ⇒ Kutopenda kwenda tena katika baa ya makaburini/mavani baada ya kuvamiwa na majambazi.

## Maudhui
**Mapuuza**
- ⇒ Semkwa, Asha na Josefina kupuuza ushauri wa Msoi wa kutoenda katika baa ya mavani kwa kuhisi jambo baya lingetokea.

**Woga**
- ⇒ Baada ya kuvamiwa na majambazi katika baa,

Asha kutoa ukwenzi mkali, ukwenzi ukafuatwa na ukwenzi, na kwenzi zikawa mjumuiko wa zogo na ghasia.

⇒ Kuna walioshangaa na kukodoa macho na kung'ang'ania kama masanamu.

⇒ Msoi kukaa akiwa ameangalia mavani.

**Itikadi/ushirikina/utabiri/uotaji/ubashiri**

⇒ Hisia zinazomfanya kutabiri maovu.

⇒ Msoi anatazamia balaa kubwa litatokea katika baa ya mavani.

⇒ Semkwa Asha na Josefina hawaamini ushirikina.

**Ujambazi/uhalifu**

⇒ Majambazi walijifanya vizuu na kuibia baa la makaburini na wateja wake kila kitu.

**Anasa**

⇒ Semkwa, Msoi, Asha na Josefina wanapenda ulevi na burudani.

⇒ Watu wanakwenda katika baa ya mavani kustarehea maisha ya dunia.

**Tahadhari**

⇒ Msoi ni mwenye tahadhari kwani siku ya mavamizi anakaa akielekea huko makaburini ili kukitokea kama alivyotabiri aweze kujinusuru.

**Ukwasi**

⇒ Msoi na Semkwa wana pesa hata Semkwa ana gari.

**Mapenzi ujanani**

⇒ Msoi na Semkwa wana wapenzi Asha na Josefina na wanakwenda kustarehe nao.

**Ulevi**

⇒ Baa ya mavani

**Ushawishi /upotoshwaji na marafiki**

⇒ Semkwa anamshawishi Msoi waende katika baa ya mavani wakati alikuwa amekataa.

Udhabiti wa msimamo

⇒ Msoi hana udhabiti wa msimamo na ndio sababu ya kushawishiwa na Semkwa kurudi mavani.

**Matumizi ya lugha**

**Tashhisi**

⇒ Kisha hisia humwotesha ndoto.

⇒ Ncha za malaika yake kusimama kama kijiti.

⇒ Leo hisia hiyo kali ilikuwa imeumuka haraka kama hamuri lililojazwa hamira.

⇒ Hutaki kuiacha(imani) ijapokuwa unajua haina haki ya kuketi wala kusimama katika maisha yetu ya kisasa ya sisi vijana yanayoendeshwa kisayansi.

⇒ Vinywaji vyake ni vya kupoza joto la wiki nzima.

⇒ Harufu za mafuta ghali na ya fahari zilikuwa zimekazana kuzikalia juu harufu za vyakula, vinywaji na za maua.

⇒ Harufu kali ya vundo la maiti ilivamia baa na kuzifurusha zile harufu nzuri za maua na manukato ya vyakula.

⇒ Vitu tawanyika, glasi na sahani anguka na vunjika- kuonyesha zogo na ghasia.

⇒ Roho yake mwaguzi inamwambia apaambae apakimbie.

⇒ Kinywaji kilipotua juu ya meza jamaa walinyanyua glasi zao-kilipowekwa.

⇒ Hata mwezi na nyota zimeshuka kidogo kuja kuimarisha furaha yetu.

⇒ Njiani Mbingu ghafla ilikasirika ikafinga uso wake mweusi kisha ikapasua mkonyezo uliotoa ufa mwembamba wa moto mwekundu na fedha, ilifanya hayo mara moja tu tena bila kutiririsha hata tone moja la **chozi**-mvua-ishara mbaya kwa Msoi.

⇒ Ama kweli itikadi na ushirikina vimekudhibiti kwelikweli.

⇒ Wanapoenda wikendi ni pa wafu na wafu wakiwa mapumzikoni wamechoshwa na kukerwa na siku yoyote ile wangefanya kitu kujihami-itikadi za kishirikina.

⇒ Imani yako imekutawala-Semkwa kwa Msoi.

**Taharuki**

⇒ Nini kinamfanya Semkwa kutumbua macho?

⇒ Baa iliendeleza huduma baada ya kuvamiwa na majambazi?

⇒ Marafiki hao walirudi tena huko?

⇒ Majambazi hao walijulikana?

**Kuchanganya ndimi**

⇒ Exotic resort-Msoi anavyopaita baa ya mavani.

⇒ u-exotic

⇒ thriller-wimbo wa Michael Jackson.

**Mbinu rejeshi**

⇒ Msoi alikuwa amenasa hisia fulani ya kitisho na wasiwasi.

**Tashbihi**

⇒ Na wewe sharti unigande mimi kama kupe-Msoi kwa Asha anapomshinikiza ale.

⇒ Ukiwa umestarehe kama vile uko peponi.

⇒ Umebaki kulala kochini kama mgonjwa wa malaria?

⇒ Jozi mbilimbili, minenguo, mikatiko, mibenuko, miondoko, mitetemeko kama wagonjwa wa malaria, mtiririko wa jasho kama maji ya mlizamu wa mto.

⇒ Kuna walioshangaa na kukodoa macho na kung'ang'ania kama masanamu.

⇒ Utabakije juu ya kochi kama mgonjwa wa homa

na leo ni jumamosi?
- ⇒ Ukiwa hapo unastarehe kama vile uko peponi mbali na adha za dunia ambako kwa tafsiri ni motoni-sitiari-uzuri.
- ⇒ Anatutisha kaka, anatutisha sisi kama watoto wadogo, anatutisha kaka-Msoi anapowaambia wataona.

**Kejeli**
- ⇒ Si baa mshenzi ya pata sote.
- ⇒ Bwana huyu naye utadhani haishi karne ya ishirini na moja-Josefina.
- ⇒ Anataka kutuvunjia raha zetu kwa ndoto zake za ajabu ajabu-takriri.
- ⇒ Kwani unatutabiria nini hasa bwana ndoto?

**Utohozi**
- ⇒ bendi hai ye msegeju-inayotumbuiza wateja.
- ⇒ Petroli-kinywaji ni petroli ya muziki.
- ⇒ kauntani-ambako wahudumu wanaenda kuchukua vinywaji.
- ⇒ glasi-bilauri
- ⇒ maisha yetu ya kisasa ya sisi vijana yanayoendeshwa kisayansi
- ⇒ wikendi
- ⇒ televisheni-waliyofungua Asha na Msoi na kupata habari-vizuu vilikuwa majambazi.
- ⇒ kochi-coach
- ⇒ swichi-ya gari la Semkwa
- ⇒ baa ya mavani

**Sadfa**
- ⇒ Imani ya Msoi wafu wangejitokeza kusadifiana na majambazi kujifanya vizuu na kuvamia baa.
- ⇒ Usiku wa mavamizi walikuwa wametembelea ile baa.
- ⇒ wimbo taribi kuimbwa.

**Balagha**
- ⇒ Una nini Msoi leo?
- ⇒ Radi ngapi zimepiga tokea dunia kuumbwa?
- ⇒ Mimweso mingapi imeemeta tokea mbingu kutandazwa na muumba?
- ⇒ Kipi cha ajabu kitakachomfanya mtu awe na hofu?
- ⇒ Imani yako imekutawala vile vile au siyo?
- ⇒ Leo Msoi umebadilisha makao? –tahadhari.
- ⇒ Umeona ukalie kiti kitakachokupa mandhari ya mava?-Asha.
- ⇒ Kwani ndiko yatakakozuka mazingaombwe unayoyatabiri?
- ⇒ Hofu hiyo itoke wapi katika usiku huu mwema uliojaa furaha na utukutu wa ujana-Msoi-kinaya-usiku haukuwa mzuri.
- ⇒ Wewe utakunywa maji kama mtoto mpaka lini?-Asha.

**Ishara**
- ⇒ Mamaya yangetokea
- ⇒ Mbingu
- ⇒ Mawingu mazito meusi
- ⇒ Radi
- ⇒ Msoi kuzitazama taa na kuziona zilikuwa na mwako wa huzuni.
- ⇒ Umeme-ishara ya mabaya.
- ⇒ Baadaye ukope wa mwezi ulistawisha uzuri wake wa fedha katikati ya vipuli vilivyokuwa vikipwitapwita-ishara ya raha kutangulia balaa.

**Takriri**
- ⇒ Duru kwa duru
- ⇒ Utapiga tena na tena
- ⇒ Anatutisha kaka, anatutisha sisi kama watoto wadogo, anatutisha kaka-Msoi anapowaambia wataona.
- ⇒ Ukwenzi ukafuatwa na ukwenzi na kwenzi zikawa mjumuiko wa zogo na ghasia.
- ⇒ Mziki ulikuwa ukitumbuiza chini kwa chini.
- ⇒ Msoi na Semkwa walifika baa ya makaburini wakati mzuri, wakati mambo ndio kwanza yaingie sura-yatengenee, yawe mazuri.
- ⇒ Msoi na Semkwa walikaa na kutazamana uso kwa uso-Msoi akelekea mavani-tahadhari.
- ⇒ Furaha, furaha, furaha imechanua raha, raha, raha.

**Taswira**
- ⇒ Majambazi waliojifanya vizuu-kundi la vizuu limejifunga kwa mtindo wa thriller wa mchael Jackson, linakuja kule baa kwa kujikongoja na kujitetemesha na kutoa sauti za kiufu, nyuso nyeupe kama chokaa, mabufuru ya vichwa yanayoning'inia hewani mabango ya nyuso yenye matundu yaliyopoteza macho na pua baadhi vimesongwa sanda vingine mwili mtupu.
- ⇒ Chakula kilikuwa ndizi za nazi pandikizi la changu wa kukaangwa pembeni na kachumbari ubavuni.

**Chuku**
- ⇒ Upeo wa raha hausemeki umekunjuliwa wazi kwa watu hawa wao wenye pesa kuukanyaga mwanzoni bila ya kufika mwisho.
- ⇒ Kwa muda mfupi mziki ukawa juu ya kila kitu.
- ⇒ mtiririko wa jasho kama maji ya mlizamu wa mto-kwa kusakata ngoma.
- ⇒ Hakucheza mpaka muziki ukamwingia damuni kama mwenyewe asemavyo kila siku.
- ⇒ Hakucheza kwa mizani ya kuchokora ndani mwili wake ili upoteze mifupa wakati wa kucheza.

⇒ Msoi kutumbua macho mpaka yakaonekana yanataka kudondoka chini kutoka vibakuli vyao-anapoona vizuu.
⇒ Msoi na Asha kukimbia bila kutazama nyuma na bila kusita pahala popote.

**Mdokezo**
⇒ Yaani umegoma…
⇒ Si mimi wala si wewe tunaoamini kwamba watu wafu wapo ndani ya dunia hii…
⇒ Si mimi wala si wewe tunaoamini kwamba watu wafu wapo ndani ya dunia hii… -tabaini

**Nidaha**
⇒ Lo, wale vizuu-Msoi akitania.
⇒ He! Saa mbili na nusu hujajitayarisha-Semkwa.

**Tanakuzi**
⇒ Mavani ni pahala pa wafu sisi sote tulichokuwa tukikiona ni kwamba mavani ni pahala pa watu hai.

**Nahau**
**Nahau**
⇒ Anaona kuna kitu kinaliza ndege mbaya-kutabiri maovu.
⇒ shingo upande, moyo mzito-Msoi akiamka kwenda kujitayarisha-bila kitaka-kujilazimisha,wasiwasi
⇒ Wakati tayari kung'oa nanga-kuanza safari kuelekea baa.
⇒ Msoi na Semkwa walifika baa ya makaburini wakati mzuri, wakati mambo ndio kwanza yaingie sura-yatengenee, yawe mazuri.

**Kinaya**
⇒ Hofu hiyo itoke wapi katika usiku huu mwema uliojaa furaha na utukutu wa ujana-Msoi akijijasirisha.
⇒ Mwezi na nyota zimeshuka kidogo kuja kuimarisha furaha yetu leo-usiku haukuisha kwa furaha.
⇒ Na tunywe tujikinge na vizuu na mashetani ya makaburini-pombe haiwezi kuwakinga.

**Mbinu rejeshi**
⇒ Miaka saba iliyopita walikuwa wamekataa kwenda baa ya mavani josefina akawAshawishi
⇒ Televisheni-matangazo ya yaliyotokea katika baa.
⇒ Semkwa kupiga simu na kueleza jinsi walivyokamatwa na majambazi na kuibiwa kila kitu, pesa, nguo, viatu hata na chupi.

**Kicheko**
⇒ Sekwa kumshika mkono Msoi anapopepesuka na kutaka kuanguka.
⇒ Wote wakaangua kicheko kabla ya kunywa.

**Koja**
⇒ Wakala, wakanywa, wakamaliza.
⇒ Jozi mbilimbili, minenguo, mikatiko, mibenuko, miondoko, mitetemeko kama wagonjwa wa malaria, mtiririko wa jasho kama maji ya mlizamu wa mto.

# 5.Kikaza

⇒ Suruai ya ndani ya aina ya pekee.

**Maudhui**
**Uongozi mbaya na athari zake**
⇒ Bwana Mtajika ni kiongozi asiyewajibika-hawezi kulinda kikaza kimepasuka.
⇒ Kwa mtajika mambo yalitendeka kindoto-kauli tupu zisizotekelezwa-ahadi za maneno.
⇒ Ni kiongozi asiyeshughulikia maslahi ya wanatekede, daima yumo ndotoni (chuku)-mwenye mapuuza.
⇒ Madharau/mapuuza-Pima kusema 'Mimi hufanya kazi yangu kikamilifu (kinaya) lakini sithaminiwi. Kila mara tumedharauliwa, tumepuuzwa na kutothaminiwa na wengine wetu.
⇒ Hawaondoi shida za wananchi baada ya kuchaguliwa-Hali huzidi kuwa mbaya si njaa, si magonjwa wala ufukara, uchochole huzidi-Bi. Chirenga-Cherehani.
⇒ Wanaacha wake wao uongozi na hawawadhibiti.
⇒ Husahau waliowachagua-wepesi wa binadamu kusahau wema na badala yake kukumbuka mabaya.

**Ubarakala**
⇒ Wadanganyifu-Machupa msemaji wa kijiji anabadilisha uongo kuwa ukweli na ukweli kuwa uongo-kutetea viongozi waovu.-ubarakala.

**Ubinafsi**
⇒ Machupa kuunga mkono hoja zinazomfaidi na nyingine kuzipinga.
⇒ Hata baada ya serikali kupinduliwa, Machupa alijua namna ya kuishi na hivyo hakuogopa chochote.-angebadili msimamo wake.

**Uwajibikaji**
⇒ Wananchi hukosa uwajibikaji katika kuchagua kiongozi anayefaa.
⇒ Viongozi kushonewa kikaza kwa ushirikiano wa umma – Wote ni washiriki katika ushonaji wa kikaza.

⇒ Hawachuji wanaotaka kuwapa uongozi, balala yake huwachagua kwa misingi ya ulumbi/umaarufu katika usemaji.
⇒ Wanapaswa kuwachagua kwa uwezo wa vitendo/kutekeleza ahadi.

- ⇒ Wengi WA wananchi hawaelewi uzito wa ushirika wao katika kushona kikaza (kuchagua kiongozi).
- ⇒ Uongozi mzuri unawategemea kwa hivyo wamchunje kiongozi vizuri.
- ⇒ Wana wajibu wa kuwaambia viongozi ukweli k.m. Babu, Cherehani na Pima.

**Mapinduzi /ukombozi/Uzinduzi/uchochezi**

- ⇒ Bi. Cherehani kufafanulia wanakijiji chanzo cha tatizo la ukosefu wa mvua.-ujasiri.
- ⇒ Bi. Cherehani kuwachochea watu waende katika ikulu wakashone kikaza kingine-kung'oa Bwana Mtajika na Bi. Mtajika mamlakani.
- ⇒ Wanatekede kuelekea katika ikulu ,Bwana Mtajika alitokea mlango wa nyuma naye Bi. mtajika akabebwa taratibu pamoja na kitanda chake akawekwa nje.

**Busara**

- ⇒ Wanakijiji kwenda kwa mzee babu kupata majibu ya masuala yanayowatatiza.
- ⇒ Wakati mwingine angewarushia maneno ya hapa na pale lakini yenye wingi wa hekima.
- ⇒ Anawapa ushauri-si kila panapo mawingu meusi mvua hunyesha.
- ⇒ Uchafuzi wa mazingira-mawingu mengine meusi hutokana na <u>**mmchafuko wa mazingira**</u>.

**Ukarimu**

- ⇒ Kila aingiaye kwa mzee babu hatoki bila kunywa angalau kikombe cha maji.
- ⇒ Wanakijiji wanatoa sehemu ya mavuno yao kwa mzee babu-umuhimu wa kuwatunza wazee katika jamii.
- ⇒ Babu anatumia **vizuri /kutunza/kuhifadhi** chakula anachotunukiwa na wanakijiji na wakienda kwake anawakirimu kwa chakula kicho hicho.

**Nafasi ya mwanamke**

- ⇒ Waiga utamaaduni wa kigeni na watovu wa maadili-wasichana wa siku hizi utawakuta wamevuta kikaza juu kwa makusudi ili macho ya wanaume yalimbuke.
- ⇒ Hapewi uongozi-nadra sana kiongozi kuwa mwanamke katika jamii ya Wanatekede.
- ⇒ Anayemdhibiti mumewe
- ⇒ Pumda wa huduma-Bi. Cherehani.
- ⇒ Waingilia uongozi –Bi. Mtajika kujiweka katika uongozi. Hata katika sherehe rasmi husahau kuwa yeye ni mkewe Bwana Mtajika .
- ⇒ Wanaowadhibiti waume wao-Bi. Mtajika.
- ⇒ Wanaojigamba- Bi. Mtajika kusema hakuna kiongozi mwingine kumshinda yeye. –majivuno.
- ⇒ Jasiri- Bi Cherehani kunena ukweli kuhusu viongozi na kuwachochera wananchi.
- ⇒ Wabinafsi-Bi. Mtajika kuwanyima wengine nafasi ya kuongea. ,

**Utovu wa maadili**

- ⇒ Wakati Bi. Cherehani anatabasamu, wengine mate yanawandondoka-kutamaani mwili wake, wakatamani ya ziada-tafsida.

**Umakini/utaratibu**

- ⇒ Mzee babu kutafuna muwa polepole na kwa ufundi mkubwa hadi kumaliza kipande chake.

**Matumizi ya lugha**

**Taharuki**

- ⇒ Baada ya mtajika na bibiye kuondolewa madarakani nani alipewa uongozi?
- ⇒ Aliyechaguliwa aliongoza vizuri?

**Nidaha**

- ⇒ <u>Lo!</u> Haitanyesha.
- ⇒ <u>Naam</u>,haya ndivyo yalivyo mambo-Pima kuhusu jinsi Bw. Mtajika alivyovunja masharti ya kikaza.

**Majazi**

- ⇒ Bwana pima-kupima kikaza.
- ⇒ Bi. Cherehani –kushona kikaza.
- ⇒ Machupa-kutokuwa na tabia nzuri-uduma kuwili, ubinafsi.
- ⇒ Bw. na Bi. Mtajika-kufahamika sana kwa sababu ya uongozi.

**Jazanda**

- ⇒ Kikaza-uongozi, madaraka, serikali.
- ⇒ Kikaza hakipaswi kushikwa kwa namna yoyote ile na mwenziwe kiongozi wa jinsia hiyo nyingine-asiingilie uongozi kwani siye alichaguliwa.
- ⇒ Washona kikaza –wananchi wanaowachagua vongozi. kumuweka kiongozi madarakani ni jukumu la watu wote.
- ⇒ Mvua nzito kunyesha baada ya wanajamii kumwondoa mtajika na bibiye madarakani-nchi kupata maendeleo au ufanisi.
- ⇒ Uzi na shindano za kushonea kikaza-katiba/sheria ambayo kwayo nchi huongozwa.
- ⇒ Kukiuka maadili ya kikaza-kiongozi kumwacha mkewe kuwa na madaraka makubwa kama kwamba yeye ndiye kiongozi.
- ⇒ Kushona kikaza kingine-kuchagua kiongozi mwingine kwa kura.
- ⇒ Mawingu bila mvua-uongozi usioleta maendeleo au usiobadili hali ya wananchi.
- ⇒ Kutonyesha kwa mvua-matatizo ya wananchi k.v. njaa, magonjwa, umaskini n.k.
- ⇒ Kijiji Tekede-nchi za Afrika-zinazoendelea.
- ⇒ Kikaza kupasuka-kiongozi kushindwa kutimiza

majukumu yake au kutowajibika kwa kiongozi.

⇒ Hurafa-safari ya kwenda mbinguni ya kobe na ndege
⇒ Kwenda mbinguni-kupata ufanisi au maendeleo/ustawi
⇒ Kobe-kiongozi
⇒ Ndege-wananchi
⇒ Ndege kumpa kobe mabawa-wananchi kumchagua kiongozi ili awaondolee matatizo na alete maendeleo.
⇒ Kope kujipa jina 'sisi wote' na kukalia vyakula vilivyoletwa na kuwakumbusha ni vya 'sisi wote' -kuonyesha ubinafsi wa viongozi au ku kujilimbikia mali wakipuuza waliowachagua.
⇒ Kobe kuwapa wenzake wanaomfaa chakula - kiongozi kuleta maendeleo katika maeneo waliyochaguliwa-mapendeleo.
⇒ Ndege kuchukua manyoya yao -wananchi kumng'oa kiongozi mamlakani.
⇒ Siku ya tano- kiongozi kuchaguliwa kwa kipindi cha kwanza cha miaka mitano na muda huo huisha bila kuleta maendeleo yoyote.
⇒ Upepo kuchukua na kubeba mawingu kuelekea kila upande mbali na kijiji-mapuuza hata mambo nyeti na kutowajibika kwa kiongozi kukosesha nchi maendeleo
⇒ Jua lililokuwa limeshika kasi kuelekea mapumzikoni <u>kama</u> kwamba linatoroka mvua lilipata nafasi ndogo ya kuwaaga wanakijiji kwa siku hiyo-kutokeza tena baada ya mawingu kupeperushwa na upepo-shida kurejelea tena kwa viongozi kutowajbika.

**Mbinu rejeshi**

⇒ Bw pima kukumbusha jinsi miaka miwili iliyokuwa imepita jinsi Bw. Mtajika alivunja masharti ya kikaza na wao kumhurumia.

**Msemo**

⇒ Walijitahidi lakini hata jitihada hufika kikomo.-kuchoka kumsitiri Mtajika kwa aibu yake.
⇒ Binadamu ni mwepesi wa kusahau wema-hukumbuka tu mabaya-kiongozi kusahau waliomchagua.
⇒ Bi chereani na Bwana Pima kuacha chungu kinatokota bila kuivisha chakula-watu wakiwa na hamu kubwa ya kufumbuliwa fumbo.
⇒ Wenye vyao na vya wengine-viongozi kujilimbikia mali.
⇒ Pole kwa wala jasho lao-wanaopata riziki kutokana na kazi za mikono yao.
⇒ Mapenzi kikoozi-mapenzi mtajika aliyonayo kwa mkewe kumfanya ashindwe kumdhibiti.

**Tashbihi**

⇒ Yanapozidi (mapenzi) huja kama nguvu za sunami-kutodhibitika.
⇒ Machupa hutafuna na hupuliza kama panya.-hula kuwili.

**Nahau**

⇒ Kumbe alitonesha kidonda-kukumbusha mambo yaliyokwisha na kusahaulika.
⇒ Tunaendelea kufanya kazi hii kwa nyoyo zote-jinsi wananchi wanavyojitolea kabisa kuchagua viongozi.
⇒ Gonga ndipo usitusimulie hadithi-sema wazi.
⇒ Wamemla mbuzi mzima na mkia utawashinda-kukamilisha kutegua kitendawili cha mawingu bila mvua.

**Takriri**

⇒ Kikaza kikaza ni cha ushirika
⇒ Mambo yana mambo yake
⇒ Ndio mtindo na sisi tunafuata mtindo
⇒ Machupa msemaji wa kijiji anabadilidha uongo kuwa ukweli na ukweli kuwa uongo

**Tabaini**

⇒ Si njaa, si magonjwa, si chochote kinachoniambaa-madhila ya wananchi
⇒ Si salamu, si chochote, hakuna kilichotoka kinywani-pima akijizuia kuongea ukweli.

**Mdokezo**

⇒ Mwafahamu katika safari ya angani namna ndege walivyoshirikiana naye…
⇒ Siri ilikuwa siri…iliwekwa na watu wawili ikahifadhika

**Kinaya**

⇒ Mawingu mazito mfululizo kwa siku tano hayakuleta mvua
⇒ Siri ilikuwa siri, iliwekwa na watu wawili ikahifadhika-hakuna siri ya watu wawili
⇒ Bi. Cherehani mwenye wingi wa soni kuweza kuongea mbele ya watu na kuwachochea.
⇒ Wanakijiji kuamini waliposhiriki hapakuwa na dosari yoyote
⇒ Kiongozi huyu alitafuta uongozi kwa muda mrefu-Kibaki

**Tashhisi**

⇒ Upepo <u>kuchukua</u> na kubeba mawingu kuelekea kila upande mbali na kijiji-mapuuza hata mambo nyeti na kutowajibika kwa kiongozi kukosesha nchi maendeleo
⇒ Jua lililokuwa limeshika kasi kuelekea <u>mapumzikoni</u> <u>kama</u> kwamba linatoroka mvua lilipata nafasi ndogo ya <u>kuwaaga</u> wanakijiji kwa siku hiyo-kutokeza tena baada ya mawingu kupeperushwa na upepo-shida kurejelea tena kwa viongozi kutowajbika.

- ⇒ Jibu lao kuibua maswali zaidi na kuzalisha kitendawili kingine
- ⇒ Ukweli ulijisukuma kwa nguvu ukafungua kinywa ambacho kwa siku chache alitembea akiwa amekiziba kwa mkono wa kushoto-pima kutovumilia kunyamazia ukweli tena
- ⇒ Hamjui ukaidi wa mkia wa mbuzi?
- ⇒ Ya kumsukuma Bi. Cherehani kiasi hiki lazima yawe mazito-ya kumlazimisha kusema lazima yawe ya muhimu sana.

Chuku

- ⇒ Kila njia ilielekea kwa mzee babu-kuonyesha jinsi walioelekea kwake walikuwa wengi
- ⇒ Pima akajizoazoa akapata nguvu, ama ni kutokana na uzito ambao ungepasua moyo wake-kutovumilika.
- ⇒ Lakini tenda lolote baya hata kama ni kuuza nzi basi litakuwa wimbo-kusisitiza usahaulifu wa mema binadamu anayotendwa na badala yake kukumbuka mabaya.

**Koja**

- ⇒ Lolote baya, litaimbwa, litachezwa ukumbini, litapandwa, litamea, litapaliliwa, litakua na hata kuvunwa.
- ⇒ Bwana pima aligundua namna ukweli unavyoweza kuumiza, kuchoma, ukandamiza na hata kunyonga.
- ⇒ Bi mtajika alijulikana. Hushangaza, akakasirisha, akaudhi.
- ⇒ Chaguo lilikuwa la kila mmoja ,ama kula, kumeza au kubugia-wanaoenda kwa babu

**Balagha**

- ⇒ Hamjui ukaidi wa mkia wa mbuzi?
- ⇒ Kwani sisi tulimchagua nani?
- ⇒ Amesema nini? –watu kuchanganyikiwa kwa kutoelewa babu aliyosema.
- ⇒ Nyote mu washiriki katika ushonaji wa kikaza itakuwaje sisi wawili tuwe na jibu la swali lenu?
- ⇒ Bwana kiongozi mbona siku hizi husemi? Haongei ili kusuluhisha hata mambo nyeti-hatoi ufafanuzi wowote hata Bi mtajika anaposema hakuna kiongozzi mwingine kushinda yeye.
- ⇒ Wangapi walio na ujasiri wa kunena ukweli hasa unapohusu uongozi?

**Methali**

- ⇒ Waliishi katika msemo wa nyani haoni kudule-wananchi kasoro la chaguo lao la kiongozi
- ⇒ Mapenzi ni kikohozi-mtajika kushindwa kudhibiti mkewe kwa ajili ya mapenzi.

# 6.Maeko

- ⇒ Mambo yanayomuweka mtu mahali
- ⇒ Mapenzi ya dhati ya Hamduni ndiyo yanamuweka jamila kwa Hamduni k.v. kumpikia, kumfulia nguo, n.k.
- ⇒ Hayo ndiyo maeko aliyowekwa huyu mwanamke. Alijikuta akistahabu maisha ya ndoa yake na Duni na akichelea kuyakosa.

**Unyanyasaji wa wanawake katika ndoa**

- ⇒ Kila aina ya matusi-mtukanifu/matusi mabaya mabaya
- ⇒ Makovu mwilini-mgongoni na mkononi
- ⇒ Athari za kisaikolojia-jeraha baya zaidi la moyo wake-moyo ulimuuma na kuatilika
- ⇒ Mateke na ngumi/kipigo

**Mapenzi ya dhati**

**Ya Jamila kwa Duni**

- ⇒ Jamila kukataa vishawishi
- ⇒ Kuvumilia ulevi, kupigwa,n.k.
- ⇒ Kukataa kushawishiwa-udhabiti wa msimamo
- ⇒ kukataa kupigana na mumewe- Ramla
- ⇒ Kukataa kumtoroka-Salim
- ⇒ Kukataa kutafuta mume mwingine
- ⇒ Kukataa kuvunja ndoa-shangazi
- ⇒ Kumbembeleza mumewe akiwa mlevi-Hai Du, wajii…onaje? Unalia nini Dii, Duni wangu? Kumpunapuna nywele na kumpigapiga vikofi vya kichwa (utu wema)
- ⇒ Kumsaidia kuchupisha mguu wake ndani.
- ⇒ kumsamehe- Hamdai chochote/hajamfanyia makosa yoyote, ni wengi wenye makosa makubwa kuliko

**Ya Hamduni ka jamila**

- ⇒ Duni Kumwandalia chai nzito ya maziwa supu na pweza, kumkaangia mayai, mandazi na chapatti, kuandika meza.-bidii, mahiri
- ⇒ Kumuinjikia maji ya kuoga
- ⇒ Kumfulia nguo
- ⇒ Ana **utu** au hisi za kibinadamu anapolevuka-anaomboleza, kulia, kuungama na kuomba msamaha na kutaka aadhibiwe.-anatambua makosa na kutubu.
- ⇒ Anamhurumia Jamila kwa kutambua kuwa simanzi na usingizi wa machovu na ukiwa wake ni kwa sababu ya kumstahimili
- ⇒ kuelekea bafuni kuoga wakirushiana mapovu na kucheka na kutaniana

**Umakini**

- ⇒ Duni kutenganisha nguo nyeusi na nyeupe, akaziweka katika mabeseni tofauti.

**Ulevi na athari zake**

- ⇒ Kurudi usiku wa manane na hivyo kusababisha Jamila kutolala vizuri kwa kukesha akimngoja.

©Bw. P.K Mwirigi (mwongozo wa Damu Nyeusi)

- ⇒ Kuathirika kiafya-kovu mgongoni, donda mkononi
- ⇒ Kuathirika kisaikolojia kutokana na maneno ya watu-kidonda moyoni
- ⇒ Kusumbua watu/majirani kwa kelele na kuwakosesha usingizi wakati wamechoka kwa kazi za mchana
- ⇒ Harufu mbaya-lile vukuto na vundo la kilevi likawa la mwanzo kuingia ndani na kuzagaa ukumbini
- ⇒ Kumpiga mkewe k.v. kumrushia teke la mbavu kwa kutopeleka chakula haraka.-ukatili
- ⇒ Kulala bila kuvua nguo
- ⇒ Kuwangwa na kichwa baada ya kulevuka siku inayofuata baada ya kulewa usiku.
- ⇒ Kutumia pesa nyingi
- ⇒ Kuchukiwa na wanajamii hata wanamtusi- mja wa laana, mlevi, mbwa, mlevi, kafiri, firauni-kudharauliwa na kupuuzwa na kutusiwa na wanajamii kwa tabia yake
- ⇒ Kushindwa kutimiza majukumu ya ndoa/kulala tu
- ⇒ Mtu hupoteza utambuzi wa jema na baya-Duni ni mzuri akiwa hajalewa lakini akilewa anageuka na kuwa mbaya -duni anafahamu kwamba usiku uliopita alimtendea karaha mkewe , ukorofi,usimbulizi n.k.
- ⇒ Kuchelewesha mke kulala akingoja mume mlevi
- ⇒ Mtu kuwa mpyaro-mwenye matusi

**Unafiki/usaliti/uchochezi/ushauri mbaya**

- ⇒ Ramla na Salim si rafiki wa kweli wa Jamila kwa ushauri wanaompa Jamila.
- ⇒ Salim rafiki wa chanda na pete wa duni anamshauri Jamila amuasi duni kisha yeye angeliweza kutoroka naye.
- ⇒ Salim kujifanya anamjua Mungu ilhali anampotosha jamila-Billahi shemeji Jamila, amini Mungu usiniamini miye.Mungu haafikiani na maovu.
- ⇒ Nakuhurumia na nakupenda shemeji kwa nini huikimbii jahanamu hii?

**Nafasi ya mwanamke**

- ⇒ Duni mbele yamwanamume
- ⇒ Mpotoshaji/mshauri mbaya
- ⇒ Mshauri mzuri kwa upande mwingine-shangazi

**Ugumu wa kubadili tabia**

- ⇒ Anaahidi kutorudia makosa lakini ni nadra kutimia miezi miwili mingine kabla ya kusikia Duni akiimba taarab-njia usiku wa manane.

**Ukombozi**

- ⇒ Watu wanaomwandama Jamila eti wanamhurumia-madhali na yeye ana mdomo na mikono anayo, akatate kuadhibiwa kama mwana asiye na kwao
- ⇒ Ramla shoga yake –neno kwa neno –watukanane, ngumi kwa ngumi-wapigane

**Ushauri mzuri**

- ⇒ Mpapurane kwa nini mwanangu?-shangazi anamshauri wasipigane (kupapurana) lakini badala yake wavunje ndoa kama haina urafiki-Madhali ndoa ni mkataba ufungao urafiki wa kitambo, basi na uvunjwe ikiwa huo urafiki haukupatikana na badala yake pana vita.

**Busara**

- ⇒ Jamila anafahamu hakuna ndoa isiyo na walakini-Ni kweli kwamba usilolijua ni usiku wa giza. Iwapi hiyo pepo nyingine katika dunia hii?
- ⇒ Analinganisha maisha yake na ya wanawake wengine-ukiona kwako kwachomeka kwa mwenzio kwateketea.

**Urembo**

- ⇒ Wengi walimtamani Jamila wamuoe-hata Salim.

**Shukrani**

- ⇒ Hata hivyo, baada ya yote alijiona anawajibika kumhimidi mola wake kwamba mume wake ameshafika salama nyumbani kwake.

**Matumaini**

- ⇒ Kamwe moyo wake haukupata kujuta wala kuacha kutaraji kuna siku mume wake angetanabahika na yale yote yakafikia mwisho.

**Ujipaji moyo**

- ⇒ Ni wanawake wangapi wa aina yake ambao wanafanyiwa anavyofanyiwa na mume wake? Wengi wao hawapati starehe azipatazo.-busara

**Nyimbo**

Wimbo wa kwanza

- ⇒ Unaangazia uajabu kwa wakaazi wa Sebleni wa Jamila kuendelea kukaa kwa Hamduni
- ⇒ Anajua msimamo wa jamila- Ameridhika kwa pendo lake

Wimbo wa pili

- ⇒ Amempa kibali awaeleze wanasebleni kinachomfanya aendelee kukaa na Duni ili waache kumtafuta au kuingilia mapenzi na ndoa yao.

Wimbo wa tatu

- ⇒ Kiitikio cha Jamila kwa nyimbo za Duni na anauimba kimoyomoyo-kilichomuweka kwa duni ni mapenzi.

**Tashhisi**

- ⇒ Sauti tu ndogo ya paka atafutaye riziki katika madebe ya taka ingeliweza kusafiri mitaa kadhaa kwa mapana na marefu-unyamavu usiku duni anaporudi

- Paka **walimuona hana thamani** mbele ya yale madebe ya taka waliyokuwa wakiyasasambura
- Sauti ilipenya katika kila dirisha na kupanda katika kila roshani ya nyumba hizi
- Siku zote ghasia na zogo la ukorofi wake **zilivuka** paa la nyumba yao na kuteremka chini-kusikika
- Sasa uso wake unabeba simanzi tupu kila wakati hata akiwa usingizini-Duni anavyomuona Jamila
- Moyo ulimwia vigumu kuusaliti-kutokubali ushauri
- Wazo lake lilivuka mipaka na kutowezekana kwa jamila-la salim
- Lile vukuto na vundo la kilevi likawa la mwanzo kuingia ndani na kuzagaa ukumbini
- Teke lilimtupa jamila kwenye kochi

Utohozi

- Ofisini-wanakofanya kazi wakazi wengi wa Sebuleni
- Bendeji-iliyofungwa kwenye mkono wa Jamila
- Kochi-jamila alikotupwa na teke la Duni
- Hoteli-alikowahi kufanya kazi duni na kupata uzoevu wa upishi
- Mabeseni-duni alikoweka nguo nyeusi na nyeupe-umakini
- Kalenda-mwaka
- kozi

**Methali**

- Dua la kuku halimpati mwewe-matusi ya wanasebleni hayakumwathiri Duni kiasi cha kumbadilisha
- Tabia haigangiki-ugumu wa kubadilisha tabia ya Duni
- Ni kweli kwamba usilolijua ni usiku wa giza-unaweza kukimbia matatizo ukakabiliwa na mabaya zaidi

**Chuku**

- Kwa kila baada ya adabu moja aliyopewa, alizidisha vituko viwili
- Alimpiga mkewe kama ngoma ya kimanga popote
- Ambao roho zawazong'ozoka mbichi kwa kukutaka-wana wapenzi makubwa kwake
- Kila aina ya tusi la ndani na nje alilijua yeye ungedhani kasomea kozi maalum yamhayo
- Almuradi kila aina ya ukorofi alikuwa nao bwana huyu akishalewa.
- Alimuona kazamisha kichwa chake kwenye mto uliorowa machozi –duni anavyomuona jamila baada ya kuamka kabla yake
- Daima usingizi wake ni wa machovu na ukiwa
- Mapishi ya duni yalimfurahisha jamila na mara zote alikuwa anajisahau kula kiasi chake, ni lazima avimbiwe tu. –uzuri wa mapishi

**Msemo**

- Mlevi si mtu-salim-kejeli

**Taswira**

- Sebleni, nyumba nyingi ni za ghorofa

**Nidaha/siyahi**

- Maskini! Jamila machozi yalimtoka-Duni kumhurumia/msikitikia kwa madhila anayopitia
- Msalie mtume mwanetu wee!
- Aste, aste baba Duni-kejeli
- Lo! Hata naye mlevi anajua thamani ya kusamehewa.
- Mwisho wa haya utakuwa lini, ya Rabi?

**Balagha**

- Hadi lini?-ataishi na mumewe mlevi/ataendelea kuvumilia
- Hadi lini Duni ataendelea kurudi nyumbani chakari na wimbo wake huu?
- Mwisho wa haya utakuwa lini, ya Rabi?
- Kwani duni alikuwa mwanamume pekee katika dunia hii ya Mungu?
- Nawe uendelee kubakia matesoni?
- Siku yenyewe ni ipi hasa?-ambayo mumewe angetambua makosa yake na kubadilika?
- Kwa nini akukongeshe mot0to ungali mbichi hapo ulipo? Kwani kakununua? -shoga
- Nipigane?
- Kama hii ni jahanamu, iwapi hiyo pepo nyingine katika dunia hii?-Jamila
- Nini teena? Kwani waadhani naataka kusaidiwa? -haoni lililo jema.
- Unasema nini Duni? Nani amekwambia kwamba mimi unanihusudi?-jamila anapomwona Duni akiathirika sana kwa anayomtendea
- Ni wanawake wangapi wa aina yake ambao wanafanyiwa anavyofanyiwa na mume wake?

**Sitiari**

- Iweje hasa kinda kama jamila …akubali kuendelea kusinginwa ndani na dume duni kama hili-mchanga-kejeli
- Kama utaweza kumkimbia shetani huyu, basi mimi niko tayari kuenda na wewe popote-chuku
- Kwa nini huikimbii jahanamu hii?

**Kejeli**

- Iweje hasa kinda kama jamila …akubali kuendelea kusinginwa ndani na dume duni kama hili
- Mlevi si mtu-Salim

Mbinu rejeshi

- ⇒ Jamila alikuwa ameolewa miaka miwili iliyokuwa imepita
- ⇒ Duni alikuwa na uzoevu wa upishi kwa kufanya kazi kama mpishi wa hoteli.-aliwahi kufanya kazi hotelini.

Tashbihi

- ⇒ Alimpiga mkewe kama ngoma ya kimanga popote apatapo-inayopigwa kwa nguvu kwa vigongo
- ⇒ Akatae kuadhibiwa kama mwana asiye na kwao

**Kinaya**

- ⇒ Pengine hii ndiyo sababu ya kuzuka wenye huruma tele nyoyo- si huruma bali ni upotoshaji/uchochezi/ushauri mbaya
- ⇒ Wimbo wa taarabu wa duni-kuwekewa zogo-yeye ndiye anawawekea wanasebleni zogo kwa mwenendo wake.
- ⇒ Kusema jamila ameridhika
- ⇒ Mapenzi kumweka jamila
- ⇒ Kuahidi angeacha ulevi na ilikuwa vigumu kutimiza miezi miwili
- ⇒ Salim kijana mtanashati ni rafiki wa chanda na pete wa duni aliye mlevi kupindukia.

**Takriri**

- ⇒ Walifika pahala pa kumshauri asikubali. Kabisa asikubali
- ⇒ Iiliokuweka oo kuweka- wimbo wa kwanza na wa mwisho
- ⇒ Meridhika oo meridhika
- ⇒ Ajibika oo ajibika
- ⇒ neno kwa neno ngumi kwa ngumi-shoga Ramla-wapigane na watukanane
- ⇒ Madhali ndoa ni mkataba ufungao urafiki wa kitambo, basi na uvunjwe ikiwa huo urafiki haukupatikana na badala yake pana vita.-shangazi
- ⇒ uduni wa duni haukuwa katika maeneo haya ya jikoni.

**Mdokezo**

- ⇒ Hai Du, wajii…onaje?
- ⇒ Kwani hata alithubutu kumgusa mkono wake, mara…
- ⇒ Watu wamelala…Haya basi sikusaidii, najua unaweza kila kitu.
- ⇒ Mja wa laana,mbwa miye mi…mi…mi…e
- ⇒ Nisamehe mke wangu…mimi mume wako, mimi … mja wa laana.

- ⇒ Imekuwa kama ni kosa kuolewa na mimi…
- ⇒ Unipige…Nipige jamila… uniue…Nilipizie halafu unisamehe
- ⇒ Imekuwa kama ni kosa kuolewa na mimi…

**Uwili**

- ⇒ Duni alizidisha vituko viwili
- ⇒ Walikuwa wameoana kwa miaka miwili
- ⇒ Mateso aliyopitia ni ya miaka miwili
- ⇒ Jamila alipoamka na kumkuta mumewe akilia, walikumbatiana na kukaa chumbani kwa muda usiopungua saa mbili

**Uzungumzi nafsia**

- ⇒ Hizi nitazifua jioni-duni baada ya kuroweka nguo za rangi nyeupe na zile nyeusi
- ⇒ Maskini mwangalie na umwone jamila hivi alivyo…maskini, mtazame sasa namna alivyobadilika wajihi wake.

**Taharuki**

- ⇒ Hatima ya Duni ilikuwaje?
- ⇒ Jamila aliendelea kuvumilia hata baada ya kuona hakubadilika?
- ⇒ Jamila alimwambia Duni kuhusu fitina ya Salim?
- ⇒ Kama alimwambia urafiki wa Salim na Duni ulikuwaje baada ya kusikia alimsaliti?

**Majazi**

- ⇒ Jamila-wema au hisani anamtendea mumewe licha ya makosa anayomfanyia
- ⇒ Duni-kitu hafifu au cha thamani ya chini-kujidunisha kwa ulevi na tabia zinazoandamana nao.
- ⇒ Sebleni-mahali m pa kupumzika nyumbani-kupumzika usiku wakati wanasumbuliwa na Duni

## 7.Kanda la Sufi

**Maudhui**

- ⇒ Mimba ile kwa Masazu ilikuwa kanda la sufi-anachukulia kuwa hawajibiki.
- ⇒ Uaminifu katika kutimiza ahadi.

**Uwajibikaji/jukumu la ulezi**

- ⇒ Babake Sela (mzee Butali) anadhani walimu pekee ndio wanapaswa kuwajibishwa kwa wanafunzi kupoteza mwelekeo lakini hata yeye anawajibika kwani lazima kuwe na ushirikiano wa wazazi na waalimu.-kuwaachia walimu majukumu yote ya kutunza watoto wa kike
- ⇒ Pia anafikiri mama ndiye aliye na wajibu mkubwa wa kumuelekeza mtoto wa kike lakini wazazi wote wawili wana jukumu sawa.
- ⇒ Mama anajua tatizo lazima liwajibikiwe na wazazi wawili.
- ⇒
- ⇒ Uwajibikaji katika /miongoni mwa vijana-wote wawili wana jukumu la kuzuia kupata mimba-Chris kumlaumu na kumnyooshea Sela kidole

kwa kumuuliza kwa nini hukujikinga

- ⇒ Sela alikuwa na wajibu wa kiutu na moyo wake uliyeyushwa na huruma alipomuona mja akiteseka.-wema uliponza.
- ⇒ Mwalimu mkuu kuwaandikia wasichana waliopata mimba barua za mapendekezo ili wapeleke katika shule za kutwa walizochagua-kuhakikisha wanaendelea na masomo
- ⇒ Mwalimu mkuu Margaret anasema kuna umuhimu wa kuwajibikia vitendo vyetu.

**Usaliti/uaminifu**

- ⇒ Rozina halati ya Kadogo si mwaminifu kwa kuwapatia Masazu na Sela Kadogo bila idhini ya wazazi wa Sela.-wanaoshirikiana na wengine kutenda maovu.
- ⇒ Masazu kutaka kukana mimba ya Sela si yake.

**Elimu**

- ⇒ Bi Margaret anathamini elimu kwa kuonelea Sela arudishwe katika shule ya kutwa
- ⇒ Mapenzi shuleni huathiri elimu ya wanafunzi hususan wasichana

**Ujinga/ulimbukeni na athari zake**

- ⇒ mapenzi hupofusha`-kuguswa sana na barua za Chris-kudanganyika kwa urahisi na kukubali kufanya mapenzi bila kinga hata bila kupimwa kubainisha kama wana magonjwa ya zinaa, kuamini kwa urahisi mtu kijana asiyemjua
- ⇒ Sela alisikia wasichana wengine wakizungumzia barua walizotumiwa na wavulana-shinikizo la wanarika

**Taasubi ya kiume**

- ⇒ Babake Sela kulaumu mama Sela anapopata mimba.
- ⇒ Kuwafukuza
- ⇒ Masazu kutumia sera kama chombo cha kujiburudisha

**Umaskini**

- ⇒ Mzee Butali kusema "Sikutumia hela zangu mimi katika elimu hadi nikaitwa pangu pakavu?
- ⇒ Sela alikaa nyumbani akikitunza kitoto katika ufukara wa pale nyumbani.
- ⇒ Mama Sela hangeweza kukinunulia kitoto nguo ilibidi matambara yatumiwe kukivisha.
- ⇒ Masazu kufanya kazi ya kuvuna mkonge na pesa anazopata zinatosha kulipa kodi na kununulia chakula.
- ⇒ Makao duni-chumba kimoja tu.
- ⇒ Umaskini wa vijana-Masazu hangemudu utaratibu wa kimila kwenda kwa wazazi wa Sela –kuasi utamaaduni.

**Tabia ya kutojali miongoni mwa wanafunzi**

- ⇒ Hawajali umaskini wa wazazi angaa wasome wainue hali yao.
- ⇒ Hawajali maisha yao ya baadaye.
- ⇒ Hawajali afya zao.

Vikwazo kwa wanaotaka kufunga ndoa

- ⇒ Urasimu wa ndoa
- ⇒ Masazu hangemudu utaratibu wa kwenda kwa wazazi wa Sela.

Ndoa haramu/ukengeushi

- ⇒ Sela kumfuata Masazu Dafina na kuishi kama mke na mume.
- ⇒ Wanaume kuishi na wanawake bila kuwa wameoana(Come we Stay).

**Uasi wa Vijana**

- ⇒ Masazu na Sela kutoomba kubali wachukue mtoto.
- ⇒ Radhi za wazazi ni fimbo kubwa ukizikosa.

**Athari ya mapenzi katika umri mdogo/shuleni/ Mimba zisizotakikana na athari zake**

- ⇒ Mapenzi ya shuleni si mara nyingi hudumu.
- ⇒ Kusababisha uzinifu.
- ⇒ Mapenzi ni matamu lakini mtu akiyapapia huwa machungu kama shubiri.
- ⇒ Hufanya mtu kuathririka kimasomo.
- ⇒ Mgogoro baina ya Sela na Masazu.
- ⇒ Mgogoro kati ya wazazi wa Sela-Sela na mamake kufukuzwa nyumbani.
- ⇒ Mzee Butali kumlaumu mkewe.
- ⇒ Sela na Kadogo kufa maji dimbwini.
- ⇒ Ndoa za mapema na haramu
- ⇒ Umuhimu wa kujitunza mtu akiwa kijana
- ⇒ Kufukuzwa shuleni.
- ⇒ Migogoro baina ya wazazi-mama kulaumiwa.
- ⇒ Hofu-maisha yangechukua mkondo gani.
- ⇒ Uavyaji mimba.
- ⇒ Kusumbua wazazi wanapoitwa shuleni.
- ⇒ Kupoteza muda wa masomo wakiandikiana au kusoma barua.
- ⇒ Kukosa utulivu.
- ⇒ Majuto-mzo wa majuto ulimwandama.
- ⇒ Kuathirika na kutoweza kutunza makini shuleni-Masazu.

**Mila na desturi**

- ⇒ Kuzuia Masazu na Sela kuoana.
- ⇒ Wanaamua kuiba mtoto kwa Masazu kushindwa kumudu utaratibu wa kawaida wa kwenda kwa wazazi wa Sela.
- ⇒ Kina mama kulaumiwa binti wakipoteza mwelekeo.

**Nafasi ya mwanamke**

- ⇒ Amepewa jukumu la ulezi-mamake Sela kualaumiwa.

- ⇒ Kumlea mjukuu wake.
- ⇒ Wanaowajibika-mwalimu mkuu.
- ⇒ Wenye mapuuza/wasiojali-Sela
- ⇒ Vyombo vya kujiburudisha vya wanaume-Sela
- ⇒ Watetezi-mama kumtetea Sela.
- ⇒ Kadogo ni kielelezo cha watoto wanaoteseka kwa ajili ya makosa ya wazazi wao.
- ⇒ Ni jasiri

**Umuhimu wa mtoto**

- ⇒ Kiungo muhimu kati ya uhusiano kati ya mke na mume.
- ⇒ Kutoa mzazi upweke
- ⇒ Kumpa mzazi shughuli

**Mapenzi**

- ⇒ Ya Masazu kwa Sela.
- ⇒ Sela kumfuata baada ya masomo waishi kama mke na mume.
- ⇒ Ya Masazu na Sela kwa binti yao Kadogo-kumwendea.
- ⇒ Mama Sela kumlea Kadogo kama mwanawe.
- ⇒ Mzee Butali kumwelimisha Sela japo ni maskini.
- ⇒ Wanakijiji kumwombea Sela na mamake msamaha kutoka kwa mzee Butali.
- ⇒ Butali anawapenda mkewe na Sela kwa kuwaonea huruma na kuwarejesha nyumbani.
- ⇒ Kumrudisha Sela shuleni.
- ⇒ Mwalimu mkuu kwa wanafunzi wajawazito.

**Ulaghai/udanganyifu**

- ⇒ Masazu kudanganya Sela kuwa ni mgonjwa-kichwa kinamuwanga.
- ⇒ Kumwarifu Sela kuwa alihisi kichefuchefu-wanapotoka katika ofosi ya sista.
- ⇒ Barua walizoandikiana ziliwasilisha ahadi za kweli na za uongo.
- ⇒ Ukiona cha mwenzio chanyolewa chako tia maji -tunaweza kupatwa na yanayopata wengine-mzee Butali hakuwahi kufikiria hali kama ile ingetokea nyumbani mwake.

**Ujinga**

- ⇒ Ulimbukeni katika mapenzi kusabaisha wasichana wengi kupata mimba wakiwa shuleni.
- ⇒ Kufanya mapenzi bila kinga ilhali wangeambukizana magonjwa ya zinaa.
- ⇒ Kukutana na mtu usiyemjua na kuishia kufanya mapenzi naye bila kujali maisha yake ya awali.

**Udhabiti wa msimamo**

- ⇒ Mzee Butali hakulegeza msimamo waondoke nyumbani licha ya Sela na mamake kulia.

**Huruma**

- ⇒ Huruma kumwingia na aliwarudisha jamaa zake nyumbani kwa majuto makuu.

**Ushauri**

- ⇒ Wazee kumshauri Butali yakimwagika hayazoleki.
- ⇒ Afanye kama alivyoelekezwa na mwalimu mkuu.

**Subira**

- ⇒ Ukosefu wa subira miongoni mwa vijana.
- ⇒ Subira katika mapenzi-ngono kabla ya ndoa.
- ⇒ Kusubiri watimize taratibu kabla ya ndoa.
- ⇒ Kusubiri wamalize masomo.

**Matatizo yanayokumba sekta ya elimu**

- ⇒ Mahusiano wa kimapenzi baina ya wavulana na wasichana.
- ⇒ Wanafunzi wasichana kupata mimba.
- ⇒ Kufukuzwa shuleni na kupoteza muda wa masomo.
- ⇒ Kuathiri wenzao na kuiga tabia kama hizo.
- ⇒ Kutojali miongoni mwa wanafunzi.
- ⇒ Ukosefu wa karo.

**Ujasiri**

- ⇒ Mamake Sela kumtetea anapofukuzwa.

**Busara**

- ⇒ Mamake Sela anajua maji yakimwagika hayazoleki.

**Unafiki**

- ⇒ Chris kuketi akiwa ameshikilia kichwa kana kwamba kingemdondoka.

Maumizi la lugha

**Chuku**

- ⇒ Kanda la sufi-mzigo wa mwenzio ni kanda la sufi.
- ⇒ Kwake usiku ule ulikuwa mwaka.
- ⇒ Mpito wa kikonokono wa wakati.
- ⇒ Masazu kusoma barua mara ya kwanza, akarudia mara ya pili na ya tatu.

**Tashhisi**

- ⇒ Mambo haya mawili yaliendelea kuungana kuhujumu mkakati wao (wakati kusonga polepole na hali ya hewa).
- ⇒ Matone ya mvua yaliyokuwa yakipenya baina ya majani ya mwembe waliojikingia mvua yalitoa sehemu yayo ya hujuma-kuwalowesha.
- ⇒ Mabasi yalikuwa yameanza kuingia huku yakiendelea kutapika wanafunzi-kuwashukisha. wanapoenda katika shule ya kina Sela ya Askofu Timotheo kulikokuwa na tamaasha za muziki na drama.
- ⇒ Saa sita usiku kiza kilikuwa kimeuma kila mahali-usiku wanaoendea Kadogo.
- ⇒ Mara nyingine maji ya kutoka mitini yalianguka kwa matone mazito na kuhujumu Kadogo.
- ⇒ Akajitahidi kujiopoa lakini utelezi miguuni ukamzidi nguvu.

⇒ Utelezi ule ukamzoa pamoja na mtoto na kumbwaga majini-kuonyesha jinsi Sela na Kadogo walivyoangamia.

**Balagha**

⇒ Huoni tayari tumesimama hapa kwa muda mrefu?-Masazu akimwambia Sela.

⇒ Kwa hiyo…?-Sela.

⇒ Huyu si mtoto wetu sisi wawili?

⇒ Je, ni kwa nini sisi huwaletea watoto shuleni?-babake Sela anamwambia mwalimu mkuu.

⇒ Mama gani anayemtazama mwana anageuka afriti ?

⇒ Sikutumia hela zangu mimi katika elimu hadi nikaitwa pangu pakavu?-kuonyesha umaskini.

⇒ Baba Sela, nani kasema huu ni msiba wangu?-mamake Sela.

**Mdokezo**

⇒ Kwa hiyo…?-Sela Masazu anapomwambia wamekaa chini ya mwembe kwa muda mrefu.

⇒ Sijambo. Sijui wewe?...sista akijibu salamu za Sela.

⇒ Rozina, Rozina, Rozinaa… amka-Sela akimwita Rozina baada ya kuona kuwa Masazu hakufaulu.

**Nahau**

⇒ Sikutumia hela zangu mimi katika elimu hadi nikaitwa pangu pakavu?-maskini.

⇒ Moyo ulimsisimka-Masazu kumuona Sela na kuingiwa na mapenzi/moyo wake kumpenda.

⇒ Kingewaborongea mkakati-kama kadogo angeamka kilio chake kingewaharibia mpango wao wa kumchukua.

⇒ Ingawa sisi hufanya tuwezayo kuwalinda wanetu, tabia zao hutupiga chenga …-hutukwepa-mwalimu mkuu anawaambia wazazi wa wasichana waliokuwa na mimba.

**Kinaya**

⇒ Shule anayosomea Sela ni ya dini ambako wanaendeleza shughuli zao kwa utulivu na ustaarabu huku wakizingatia maadili ya hali ya juu ilhali Sela anapata mimba.

⇒ Shule anayosomea Masazu inaitwa lenga juu ilhali analenga mapenzi na kutia wasichana mimba.

⇒ Sela kupata mimba licha ya babake kuwa mkali.

⇒ Sela kupata mimba licha yake kuonekana kuwa msichana anayewajibika.

**Utohozi**

⇒ Drama-michezo ya kuigiza

⇒ Mabasi ya shule ngeni

⇒ Kliniki- mahali pa wanafunzi kutibiwa shuleni.

⇒ Sista-daktari wa kliniki aliye mtawa wa kikatoliki.

⇒ Ofisini-ya sista daktari

⇒ Glasi ya maji-aliyopeewa Masazu kumezea vidonge viwili.

⇒ Kiberiti cha gesi-hewa iwakayo moto cha Masazu cha kuwashia sigara anachotumia Masazu kumulikia.

**Tashbihi**

⇒ Kama chui aliyelivizia windo lake na sasa limetokea, akajiandaa-Masazu anapomwona Sela katika pitapita zake katika shule ya kina Sela na kujiandaa kumtongoza.

⇒ Alitunza barua ile kama uhai-Sela iliyokuwa imepuliziwa maashi-chuku pia.

⇒ Kiapo cha Masazu-kuchomeka kidole chake cha shahada ardhini na kumwambia mapenzi yake kwake ni ya dhati ) kikalegeza kiwiliwili chake (Sela) mithili ya mbwa anayekabiliana na chatu macho kwa macho-kumfanya akubali penzi.

⇒ Ulimwengu ulivurugika, akawa kama tiara inayopeperushwa na upepo ikaenda arijojo.-Sela kuathirika kwa kupata mimba.

**Nidaha**

⇒ Pole Chris-akimliwaza kwa maumivu.

⇒ Kijusi kilikuwa kimetungika!-Sela alikuwa na mimba.

⇒ Naam, naam shemeji Masazu-Rozina akimwitika Masazu.

⇒ Ahsante-Masazu akimshukuru Rozina.

**Sadfa**

⇒ Sela anapotaka kuingia kwa sista kumwarifu kuhusu Masazu naye sista alikuwa akitoka.

⇒ Hapakuwa na wanafunzi wengine katika kliniki ndiposa Masazu akaweza kumtongoza Sela.

Kupitapita kwa Masazu katika shule ya Askofu Timotheo kusadifiana na Sela kutokea ambaye moyo wake unampenda.

**Tanakali**

⇒ Alikataa katakata-kurudi katika zahanati Sela anapohofu angezidiwa.

⇒ Kroo! Kroo! Kroo! Za vyura usku wa kuendea Kadogo.

⇒ Pata pata pata! Masazu na Sela wakipita kwenye maji na matope wakirudi baada ya kumchukua Kadogo.

⇒ Kadogo alikuwa amelala fofofo alipoendewa.

**Sitiari**

⇒ Barua ile ilikuwa parafujo fulani moyoni mwa Sela-ilimgusa sana kwa kutowahi kupokea barua nyingine kutoka kwa mvulana.

⇒ Boma la mzee Butali kugeuka na kuwa jahanamu-kuwa na zogo na fujo baada ya kutoka shuleni.

**Methali**

- ⇒ Yajapo yapokee-Chris kwa Sela-si tatizo lake-halimhusu.
- ⇒ Mimba ile kwa Masazu ilikuwa kanda la sufi-mzigo wa mwenzio ni kanda la sufi.
- ⇒ Mpango uliokuwapo ulikuwa usiku wa giza-Sela na wasichana waliokuwa na mimba kutojua hatima yao baada ya kuelekezwa wasubiri katika chumba cha mapokezi.
- ⇒ Uchungu wa mwana, aujuaye ni mzazi-mamake Sela.
- ⇒ Maji yakimwagika hayazoleki-alielewa baada ya ushawishi wa wazee.

**Kicheko/tashtiti/kejeli**

- ⇒ Vicheko vya chini kwa chini vilianguliwa na wanafunzi.

**Ishara**

Giza- tanzia ambayo ingetokea-Sela na Kadogo kufa maji kwa kutumbukia kidimbwini.

**Takriri**

- ⇒ Rozina, Rozina, Rozina! Masazu akimwita halatiye Kadogo usiku ule wamemwendea Kadogo.na Sela.

**Taswira**

- ⇒ Ilibidi matambara yatumiwe kukivisha kitoto-kuonyesha umaskini wa wazazi wa Sela.
- ⇒ Walifika mahali mti ulikuwa umeanguka na majani kukingama njiani.
- ⇒ Mara wakafika sehemu ambapo njia ilikuwa pana lakini kulikuwa na jiti lililoangushwa katikati.
- ⇒ Palikuwa na dimbwi la maji lililotuama pale.
- ⇒ Akawa tayari keshaelekea pale na kujikuta katia mguu majini, yamemzagaa na kumfika magotini yanatishia kumsomba.

**Mbinu rejeshi**

- ⇒ Tunaelezwa jinsi mapenzi kati ya Sela na Masazu yalipoanza wakati wa tamaasha za muziki na drama katika shule ya kina Sela.

**Sadfa**

- ⇒ Sela na sista kukutana mlangoni wakati amempeleka Masazu akatibiwe.

**Utatu**

- ⇒ Sela na mamake kukaa kwa jamaa yao kwa majuma matatu.
- ⇒ Sela kukaa nnyumbani kwao kwa muda wa miezi mitatu akitunza kitoto chake.
- ⇒ Majina ya wanafunzi watatu kuitwa na mwalimu mkuu wafike ofisini mwake.

**Taharuki**

- ⇒ Masazu alifaulu kuwaokoa Sela na Kadogo?
- ⇒ Alipofaulu kuwaokoa walikuwa wafu au wazima?
- ⇒ Au wote watatu walikufa maji?
- ⇒ Rozina aliwaambiaje wazazi wa Sela baada ya kuamka na kukuta Kadogo hakuweko?
- ⇒ Masazu aliwafahamisha wazazi wa Sela kuhusu maafa yaliyotokea?

# 8.Shaka ya mambo

**taharuki**

- ⇒ Kutokuwa na uhakika wa jambo au jambo la kutuhumiwa.
- ⇒ Kuna shaka ya mambo kama Esther aliendelea na masomo kwa kusomea usekretari kwani hana pesa.
- ⇒ Kama Kamata alikuwa anampenda yeye au alikuwa na mapenzi na Grace.
- ⇒ Ukaribu kati ya Kamata na Grace ulikuwa wa kutia shaka.
- ⇒ Esther alitoka kwa mzee Mwinyi na kwenda kupanga chumba chake?
- ⇒ Alihama madaraka na kupanga nyumba yao na Kamata?
- ⇒ Alibadilishiwa zamu na Grace?
- ⇒ Miadi muhimu sana aliyonayo Grace ni ya kutiliwa shaka.
- ⇒ Shaka kama Grace na Kamata walikuwa shule moja na iwapo waliishi Buruburu na wazazi wao.
- ⇒ Mtu ambaye Grace anaenda kukutana naye ni Kamata au mtu mwingine?
- ⇒ Yawezekana ndio walipanga abiria aende mkahawani wamshtue kwa tangazo aharakishe asahau pesa?
- ⇒ Shaka kama Kamata alimpata abiria aliyeacha bunda la pesa au ndege ilikuwa imeondoka.
- ⇒ Kama Grace na Kamata walimpatia mzungu pesa walizopatiwa na Esther.
- ⇒ Kama Grace alikuwa anapewa lifti tu na Kamata au walikuwa na mpango wa kwenda kustarehe pamoja kama wapenzi.
- ⇒ Kama Kamata anampenda Esther jinsi Esther anavyompenda kwa kutompitia Esther mahali pa kazi na kutopokea simu zake hata kuzikata.
- ⇒ Kuna shaka Grace anapomwita Kamata mpenzi kama ni utani tu au ni kweli. Kamata anamkonyezea jicho.
- ⇒ Shaka kuwa anakataa kumbadilishia zamu ali apate muda mwingi wa kuwa na Kamata.
- ⇒ Shaka Grace anapomwomba Esther aendelee na zamu yake hadi usiku ana miadi muhimu sana Nairobi-ni ukweli au ataka wakutane na Kamata?
- ⇒ Shaka kuwa Grace kutobmbadilishia zamu kama anapenda kufanya kazi hadi usiku ama

anataka wawe pamoja na Kamata.

⇒ Kuna shaka kwa nini Kamata anakataa waende disko na Esther badala yake waende katika vilabu kama huko ndiko hata Grace anataka apelekwe na Kamata hataki wakutane.

⇒ Kuna shaka ya Kamata kukata simu ya Esther kama ni kwa kutotaka aijibu wakiwa na Grace asije akajua ana mpenzi mwingine.

**Umaskini**

⇒ Familia ya Grace kushindwa kumsomesha kozi ya uhazili na kuachiwa jukumu la kujisomesha mwenyewe.

**Heshima/utu wema**

⇒ Mvulana kumwinukia Esther kiti na kumkaribisha akae katika matatu akielekea kazini.

⇒ Esther kumshukuru kwa kusema , "Ahsante'.

**Balagha**

⇒ Ugeni au usasa gani?-heshima ya kuinuka huitwa na watu wengine usasa.

⇒ Kwani zamani wavulana hawakuwapa heshima wasichana?

⇒ Hicho ndicho kitu kigeni hapa Afrika?

⇒ Kamata anampenda kwa dhati?

⇒ Kamata kweli anamjali au naye anshughulika kutafuta pesa?

⇒ Kweli Kamata angeinuka na kumpisha yeye Esther kiti?

⇒ Sasa upo ulakini hapo?

⇒ Kazi gani hii ya kuamka alfajiri siku sita kwa wiki na kujisukuma garini macho yamejaa usingizi?

⇒ Sijui amekuja kazini leo? -kukaribia saa sita na Kamata hajafika hajafika.

⇒ Anaumwa?

**Ujinga**

⇒ Esther kuamini Kamata angempa abiria asiyemjua pasa ilhali hajamweleza wasifu wake.

**Unafiki**

⇒ Grace kusema Kamata atampa lifti na hataki amcheleweshe.

⇒ Kamata kumwambia Grace atangulie kwenye gari na akishampa abiria pesa angeenda waondoke.

**Ulaghai/udanganyifu/utapeli**

⇒ Kamata ni tapeli wa mapenzi na pesa.

⇒ Kamata kusema apewe pesa ampelekee abiria na abiria wapo hapo.

⇒ Grace kumwambia Esther ampe Kamata pesa ampelekee.

**Subira**

⇒ Anataka Kamata astahimili kidogo, lakini ndio hivyo, wanaume hawana subira .

⇒ Vijana hawana subira. Esther anataka waishi pamoja na Kamata kama mke na mume kabla ya ndoa.

**Anasa/starehe**

⇒ Esther ana hamu ya kuenda na Kamata disko kama wafanyavyo vijana wengine.

⇒ Kamata anashughulika na kutafuta pesa na starehe.

**Madhira ya abiria wa ndege**

⇒ Kucheleweshwa.

⇒ Safari kuahirishwa.

⇒ Kutosikia safari zao zikitangazwa na watangazaji kutisha abiria kimakusudi.

⇒ Kufanya kazi muda mrefu-siku sita kwa wiki

**Tamaa**

⇒ Esther ana tamaa ya pesa asomee usekretari.

⇒ Kamata ana tamaa ya wasichana.

⇒ Kamata na Grace wana tamaa ya pesa ndiposa wanatumia ulaghai kupata pesa zilizoachwa na abiria.

**Uhuru**

⇒ Esther anataka asomee usekretari kazi itakayokuwa na uhuru zaidi.

⇒ Amekuja Nairobi kutafuta uhuru lakini mzee Mwinyi anamchunga kama mtoto.-yeye ni amana yao-kitu cha thamani mtu anachopewa na mwingine ili amtunzie-udhibiti wa mwanamke-kuchungwa ili wasiharibike kitabia.

**Uaminifu**

⇒ Kamata si mwaminifu kwani ana mpenzi mwingine zaidi ya Esther anayeitwa Grace aliye mkuu wa Esther kazini katika mkahawa ulio katika uwanja wa ndege.

⇒ Grace amekosa kumtimizia Esther ahadi ya kumtoa zamu ya kuanzia asubuhi saa kumi na mbili –angembadilishia zamu kila mwezi wa pili na angeingia kazini mchana saa nane na kutoka usiku.

⇒ Esther ni mwaminifu kwa vile mteja anaposahau pesa anazishika upesi na kutoka mkahawani kumpelekea lakini hamuoni.

⇒ Ni mwaminifu katika mapenzi kwa vile anampenda Kamata anamfikiria na kupanga watakavyoishi baadaye naye.

**Ukarimu**

⇒ Esther kumshikia Grace zamu yake.

**Ukengeushi**

⇒ Vijana kuishi pamoja kama mke bila kuwa wameoana.

**Utamaaduni**

⇒ Wanawake hawaheshimiwi na kuwaheshimu ni

usasa.

**Matatizo ya wafanyakazi**

⇒ Kuamka alfajiri siku sita kwa wiki na kujisukuma garini macho yangali yamejaa usingizi.
⇒ Kutobadilishiwa zamu.
⇒ Hangeuliza kwani angefanya hivyo angefikiriwa kuwa mtu matata.
⇒ Mishahara duni.

**Matumizi ya lugha**

**Tashhisi**

Mvua ya siku iliyopita ilimbembeleza na kumlaza usingizi mtamu.

**Kuchanganya ndimi**

⇒ Jommo Kenyatta international airport-anakofanya kazi Esther.
⇒ Mombasa road -barabara gari lililoingia.

**Utohozi**

⇒ Usekretari-uhazili ambao Esther angesomea baada ya kupata pesa za kutosha.
⇒ Kupiga taipu
⇒ Kompyuta
⇒ Dola elfu-kiasi cha pesa ambacho Esther alikisia abiria aliacha.
⇒ Huduma za kiofisi
⇒ Kaunta –ya mkahawa
⇒ Airport-uwanja wa ndege
⇒ Nambari-ya gari
⇒ Lifti-ambayo Grace anadai anapewa na Kamata
⇒ Tiketi
⇒ Disko-ambako Esther ana hamu ya kwenda na Kamata
⇒ Wiki-anafanya kazi siku sita kwa wiki.
⇒ Dola hamsini-ambazo zilitakikana chuoni kama rubuni ili Esther aweze kusomea kozi ya uhazili

**Mbinu rejeshi**

⇒ Esthre alitoka kwao miezi mine iliyopita na kwenda Nairobi.
⇒ Babake Esther alikuwa akifanya kazi Nairobi miaka ya sabini.Aliamua kurudi kwao baada ya mzee Jommo Kenyatta kufariki mwaka wa 1978, miaka mitano kabla ya Esther kuzaliwa.

**Tashbihi**

⇒ Anachungwa kama mtoto kama alivyochungwa nyumbani.

**Takriri**

⇒ Lakini pesa! Kila kitu pesa.
⇒ Mtu hawezi kupiga hatua duniani bila pesa. Kuzaliwa kunahitaji pesa. Kuolewa pesa. Kuzaliwa kunahitaji pesa.

**Msemo**

⇒ Wanaume hawana subira

**Kicheko**

⇒ Esther kumuuliza Grace kama ana mpenzi akicheka.
⇒ Grace kucheka anapoulizwa hivyo.

**Mdokezo**

⇒ Ndiyo nimebahatika lakini…-Esther akiwaza-kupata usafikiri kumpeleka hadi kazini.

Hapana n'na mengi ya kufanya kabla ya kukutana na … kabla ya miadi yangu-Grace anapoambiwa na Esther itakuwa mapema.

⇒ Esther, sina wakati. Mimi lazima niondo…

**Taswira**

⇒ Kamata kutokea akiwa amevaa suti ya bluu, shati la manjano hafifu na tai ya kijivujivu, uso wake uking'ara kwa furaha na pia kwa kupakwa mafuta ya kulainisha ngozi.

**Nidaha**

⇒ Kamata! Hajui anamfikiriaje yeye Esther.

**Taharuki**

⇒ Kamata alipokuwa hapokei simu ya Esther kwa kuikata au kuacha ikatike?
⇒ Alikuwa wapi?
⇒ Kamata alifanikiwa kumpata mteja aliyesahau fedha?
⇒ Esher aligundua uhusiano uliopo kati ya Kamata na Grace?
⇒ Kama aligundua alifanyaje?
⇒ Hisia zake ziliathirika kiasi gani?
⇒ Esther alifanikiwa kutimiza ndoto yake ya kusomea usekretari?

# 9.Maskini babu yangu

⇒ Maskini-kihisishi cha kuonyesha huruma
⇒ Kuugua-kushikwa na maradhi Fulani uzeeni.
⇒ Kusingiziwa kuwa mwizi wa mtoto
⇒ Kusingiziwa kuwa mchawi
⇒ Kupigwa, kuuawa na kuteketezwa na umma.

**Utamaduni**

⇒ Watantele wanawake kujitandia mitandao na kuvalia mavazi marefu yaliyositiri maradufu viwiliwili.

**Utabaka na athari zake**

⇒ Sakata ina makabila mawili tu, maskini na matajiri
⇒ Watu wa mjini na watu wa shambani
⇒ Huduma bora za kijamii zinapatikana mijini kama vile hospitali bora.

**Ubandia wa uhuru**

⇒ Haukuleta manufaa kwa watu wote

**Uozo**

⇒ Ukabila, ufisadi na hongo babu anasema ni

vipengee halisi vya maisha ya binadamu.

**Bidii**

⇒ Babu kutotaka kuacha mifugo wake aende akatembee mjini. Alitembea kwa kuraiwa sana.

⇒ Idili ya babake katika jeshi la polisi kusababisha apandishwe cheo hadi mrakibu wa polisi.

**Ndoa**

⇒ Kati ya watu wenye asili mbalimbali.

⇒ Ndoa ya babake na mamake msimulizi kupingwa na pande zote mbili.

**Heshima kwa wazazi**

⇒ Babake msimulizi anajali babake kwa kumchukua kuja kutibiwa mjini.

**Ubaguzi**

⇒ Ndoa kati ya Watantele na Wamindi na makabila mengine nchini subu ni nadra.

⇒ Ndoa ya babake na mamake msimulizi kupingwa na pande zote mbili.

⇒ Babu Maende na babu Tandeka, mama-Zuhura Kimbaumbau.

⇒ Wazazi hawana ubaguzi-kuna maelewano kati ya mababu na bibi na babu kutembeleana

**Umaskini**

⇒ Mtaa wa Madongo, eneo la Kochokocho kuwa na watu wa asili mbalimbali.

⇒ Hali zao za maisha ni duni.

⇒ Taswira ya nyumba

⇒ Wanawake kukaanga samaki kandokando ya barabara na kuwauzia wapita njia.

⇒ Kina mama kuuza chapatti zilizokaukiana  na mandazi makavu.

**Ukatili/uchukuzi wa sheria mikononi**

⇒ Msimulizi ana nywele za singasinga.Wakitembea mitaa ya Kochokocho wanavamiwa na Watantele.

⇒ Walipaswa kumpeleka babu Maende kwenye vyombo vya sheria ili ibainike kama alikuwa amefanya makosa.

⇒ Alisingiziwa kuiba mtoto na kumloga-Mtoto mtantele umemtoa wapi? Wee! Waacha! Unawezaje kumpata mjukuu wa kitantele? Mchawi huyu amemroga mtoto mpaka akamwita babu yake. Mwizi wa mtoto!

⇒ Kumpiga, kumuua na kumteketeza- Mama mmoja kumnyaka kibao shavuni, Mchomeni moto. Mwekeni tairi!

**Matatizo ya uzeeni**

⇒ Babu kushikwa na maradhi fulani ya uzeeni.

**Ujasiri**

⇒ Babake na mamake msimulizi wanavunja miiko ya kutoolewa na kabila lingine.

⇒ Wanapinga mila potovu na kuanzisha ujenzi wa jamii mpya isiyo na ubaguzi.

**Utamaduni**

⇒ Mamake kukulia Kisubu na kuimba nao nyimbo za kitamaaduni.

⇒ Huko madongo msimulizi aliwaona wanawake waliojitandia mitandio na kuvalia mavazi marefu.

**Matumizi ya lugha**

**Mbinu rejeshi**

⇒ Mamake msimulizi Zuhura kimbaumbau ni Mtantele kutoka Kitolo. Walihamia nchi ya Sakata huko Kabucheka kituo cha biashara miaka ya sitini. babake alikuwa na duka la reja reja-kuonyesha msimulizi ana usuli mseto babu Maende kuumeni na babu Tandeka kuukeni.

⇒ Msimulizi anatukumbusha Jumamosi babu yake aliuawa wakiwa naye.

⇒ Katu sikutaka kukumbuka… Miaka ishirini imepita tangu yalipotokea yaliyotokea.

⇒ Rekodi za santuri-alikosikia babu mtaa wa kochokocho ukiimbwa ndipo akataka wakautembelee.

**Takriri**

⇒ Sikutaka kutazama <u>nyuma</u>, kupiga darubini <u>nyuma</u>, kukumbuka <u>nyuma</u>.

⇒ Kila <u>siku</u>, kila <u>siku</u> kochokocho-wimbo wa rekodi.

⇒ Nilijiwaza kwamba <u>hayakuwa yalikuwa, yalikuwa hayakuwa</u>-yalitokea au hayakutokea.

⇒ Yale <u>yamesimama yamesimama</u> wima yamesimama wima kwa rehema za Mungu

**Nahau**

⇒ <u>Kujitonesha donda</u> akitazama nyuma-kujikumbusha msiba uliokwisha na kusahauliwa.

⇒ Shikia shokoa-babake msimulizi <u>alimlazimisha</u> babu aingie katika gari la Toyota Corolla ampeleke mjini hospitalini

⇒ Nilipiga unyende-msimulizi <u>kupiga mayowe</u> kwa kuona babuye akishambuliwa na umati.

⇒ Jamani! Jijini kuna maisha ya <u>kukatisha tamaa</u> sana.-babu alipoona umaskini wa madongo-kupotezesha matumaini.

**Tashhisi**

⇒ Donda ndugu lililokataa kusikia dawa-kisa cha mauaji ya babu yake <u>kuosahaulika</u>.

⇒ Shinikisho la wenzangu kutaka niandike <u>limenisakama</u> kupindukia-<u>kumlazimisha.</u>

⇒ Nyumba yetu <u>kutawaliwa</u> na vicheko, tabasamu-furaha babu anaposema amepata nafuu kiasi.

⇒ Wauzaji kuwa na kazi kubwa kuliwinga wimbi kubwa la nzi <u>waliotaka</u> kula uhondo-hali ya

uchafu katika soko huko madongo.
- ⇒ Mtaa wenye mabanda yaliyoinamiana na kuoneana imani.
- ⇒ Yale yamesimama yamesimama wima yamesimama wima kwa rehema za Mungu
- ⇒ Ukata uliokuwa umewafunika na kuwafanya wa kabika moja la wachochole.
- ⇒ Kuta za mbavu za mbwamabati yaliyojifunika libasi ya kutu.

**Majazi**
- ⇒ Kochokocho-mahali kuliko na vituko vingi hasa eneo la Madongoporomoka.
- ⇒ Madongoporomoka-kwenye nyumba za udongo ambazo hubomoka hasa wakati wa mvua-makao duni-umaskini.

**Mdokezo**
- ⇒ Donda ndugu lililokataa kusikia dawa…

**Chuku**
- ⇒ Sakata ina makabila arobaini kama wengine waaemavyo, yapo makabila mawili tu, maskini na matajiri.
- ⇒ Ukata uliokuwa umewafunika na kuwafanya wa kabika moja la wachochole.-hali mbaya ya umaskini.
- ⇒ Meno yangu karibu kudondoka kwa hasira nilizokuwa nazo nikijaribu kumtafuna mwanamke aliyemnyaka babu kibao shavuni.
- ⇒ Mnuko ulioweza kulipua pua-harufu mbaya huko madongo.
- ⇒ Kitanga changu cha mkono kilizama katika bahari ya kitanga chake (babu) kikubwa.
- ⇒ Mabanda-labda yanaweza kuanguka kwa upepo wa mtu apigaye mbinja-kuonyesha udhaifu wayo.
- ⇒ Kidimbwi cha jasho kikawa kinajisawiri kwenye ncha ya mwanzi wa pua yake-babu kuogopa.
- ⇒ Nilipiga unyende nikalia machozi mpaka yakanikauka.
- ⇒ Ndoa ya babake na mamake msimulizi ilikuwa ndoa moja katika maelfu.-kuonyesha ubaguzi, ukabila.

**Methali**
- ⇒ Yaliyopita hupishwa-anaonelea anastahili kusahau tanzia ya babuye.
- ⇒ Kinolewacho hupata-mama yake kurithi mila za Wasubu.

**Utohozi**
- ⇒ Ekari tano-shamba babu yake alilomiliki
- ⇒ Mwekeni tairi-gurudumu ili achomwe.
- ⇒ Hospitalini-mjini ambako babu alipelekwa akatibiwe

**Balagha**
- ⇒ Kwao wapi?-babu
- ⇒ Kwao mashambani au vijijini?
- ⇒ Yaani mtu kwao hakuwezi kuwa jijini?
- ⇒ Mtu atasemaje haya ninayosema kuhusu mama yangu ni uongo?
- ⇒ Mama yangu hakuwa mtoto wa Kitantele aliyelelewa katika mazingira yaliyomzunguka na kunga na kaida za Wasubu?

**Mdokezo**
- ⇒ Ingawa mimi nilifurahi hadi… -msimulizi kufurahi babu alipopelekwa mjini akapelekwe hospitali ya jiji.
- ⇒ Unyende wangu ulipotelea kwenye mzozo uliotokota nje…

**Tashbihi**
- ⇒ Wamindi kuoana na makabila mengine hutokea kwa tukizi kama kupatikana kwa mwanasiasa mwadilifu. (uongozi mbaya)
- ⇒ Vilango vilivyosimama vizingitini kama vibua vya mtamaa vinavyosubiri kuanguka.-makao duni
- ⇒ Ulimi wake ulikuwa mwepesi kusarifu kisubu kama mwenyeji-wa mamake msimulizi.

**Taswira**
- ⇒ Tope jeusi, vichochoro kujaa tope, fodogoo na kila aina ya uozo-uchafu mwingi.
- ⇒ Mabanda yaliyoinamiana na kuoneana imani
- ⇒ Kuta za mbavu za mbwa, mabati yaliyojifunika libasi ya kutu.
- ⇒ Kina mama kuuza chapatti zilizokaukiana na mandazi makavu na maembe dodo.
- ⇒ Vitoto vingi vya maji ya kunde. Viwili vitatu ndivyo vilikuwa vyeusi kuliko masizi ya chungu cha nyanya wa kabucheka.

**Nidaha**
- ⇒ Salaala! Mbona wasirudi kwao wakaishi maisha ya maana kidogo?
- ⇒ Jamani! Jijini kuna maisha ya kukatisha tamaa sana.-babu alipoona umaskini wa madongo

**Utohozi**
- ⇒ Rekodi za santuri-alikosikia babu mtaa wa kochokocho ukiimbwa ndipo akataka wakautembelee.

**Tabaini**
- ⇒ Si siahi, si mayowe, si miluzi almuradi fujo moto mmoja.

**Taharuki**
- ⇒ Kwa nini kina mama wanaofanana na msimulizi wanamtumbulia macho kama waliona kioja?
- ⇒ Nini kilifanyika baada ya babu kuuuawa?
- ⇒ Wauaji walijulikana?
- ⇒ Walichukuliwa hatua gani?

⇒ Hatima ya ndoa ya wazaziye msimulizi ilikuwaje baada ya kukataliwa?
⇒ Msimulizi alijulikana alikotoka vipi baada ya babu yake kuuawa?

**Kinaya**

⇒ Baba ya msimulizi ni mrakibu wa polisi ilhali baba yake anauawa kinyama kwa kupigwa na kuchomwa moto.
⇒ Babu Maende japo anaugua ilhali hataki kwenda Pilka kutibiwa bali alilazimishwa.
⇒ Kuuawa baada ya kupona ugonjwa uliomleta siku moja tu kabla ya kurejea kwake.
⇒ Kuambiwa ndoa ilipingwa na pande zote mbili kisha kuna maelewano kati ya mababu na bibi na babu kutembeleana.

# 10.Ndoa ya samani

⇒ Ndoa kutojengwa kwa misingi ya mapenzi ya dhati bali mali-samani.
⇒ Kuangalia mtu badala ya utu.
⇒ Abu anaghairi kumwoa amali na kurudi Arabuni.
⇒ Wazazi kuingilia ndoa za watoto na kuishia kuzivunja kwa tama zao.
⇒ Umaskini kuwa kikwazo cha mafanikio ya mtu.
⇒ Matatizo ya ndoa za matabaka tofauti.-utabaka kuwa kikwazo katika ndoa.

**Utabaka**

⇒ Kijijini kulikuwa na watu tajiri na maskini- Kina Abu ni maskini na kina Amali ni wa tabaka la kati-si maskini wala tajiri.

**Ujinga**

⇒ Amali kufanyiwa maamuzi na mamake yanayoishia kumponza.
⇒ Kumfilisi mwamamume anayekusudia kuolewa naye.
⇒ Kutojua tamaa mbele mauti nyuma

**Utunzaji**

⇒ Abu kutotapanya mali aliyoipata.

**Unyenyekevu**

⇒ Ukwasi haukumpa takaburi.

**Ukarimu**

⇒ Kuwajengea wazazi nyumba nzuri. (anaheshimu wazazi).
⇒ Kutoa mahari kabla ya kuoa.
⇒ Kusaidia baadhi ya jamaa kupata kazi arabuni
⇒ Kuwaajiri marafiki

**Ubinafsi**

⇒ Mamake amali kutohusisha wazazi wa abu katika mipango ya arusi.
⇒ Kutofikiria maisha ya bintiye bali ataka ajipatie mali.

**Bidii**

⇒ Abu anatufahamisha hakuwa mzembe.
⇒ Alifanya kila sambuli ya kazi.
⇒ Akajijengea chumba cha msonge kilichokandikwa kwa udongo. (taswira)
⇒ Akaweza kujipatia chakula na kujinunulia nguo.
⇒ Arabuni anafanya kazi ya uhamali ambayo inamtajirisha.

**Tamaa**

⇒ Ya mama Zena mamake Amali

**Upuuzaji wa majukumu**

⇒ Babake Amali mzee Kadiri kutomdhibiti mkewe na kutotoa kauli yake.

**Utamaushi**

⇒ Nilitamauka-kukata tamaa baada ya posa yake kukataliwa.

**Utamaaduni**

⇒ Mila ya mahari kuwa kikwazo cha vijana kufunga ndoa kwa sababu ya umaskini.
⇒ Mjomba kuhusishwa katika suala la ndoa.
⇒ Nyimbo za ndoa
⇒ Utozaji wa bwana arusi pesa aendapo kumchukua bibi arusi.

**Nafasi ya mwanamke katika jamii**

⇒ Chanzo cha matatizo ya mwanamke mwenzake au kikwazo cha mafanikio yao.
⇒ Wana usemi/sauti-babake amali kushauriana na mama zena anapoelezwa na mjomba wa Abu lengo la ujumbe wao.
⇒ Mfanya maamuzi badala ya mwanamme au wanaodhibiti waume zao- “Amali hataki kuolewa, tena sijui kama utaweza mahari.” (waongo)
⇒ Yoyote yaliyoamriwa kwake babake Amali yalikuwa mamoja.
⇒ Nyenzo ya kiuchumi
⇒ Wapotoshaji-kumpotosha amali aitishe mali
⇒ Kiumbe duni kisichoweza kujidhibiti-babake kutaka amali aolewe asizalie nyumbani.
⇒ Wananyimwa haki ya kujiamlia mambo yao.
⇒ Wabaguzi
⇒ Wabinafsi
⇒ Wana tamaa, wapenda makuu-mama Zena.

**Imani kwa Mungu**

⇒ Abu baada ya posa yake kukataliwa na kuamua kusahau mambo ya kuoa alimwomba Mungu ampe mke mwema ambaye angempenda jinsi alivyo.

**Uadilifu**

⇒ Mwone mtoto amejihifadhi katulia kwao wala si kiguu na njia-Amali.

**Ulevi**

⇒ Fahami na jamaa wengine walikuwa wakifaidi mairungi-miraa-alipomwambia waende nyumbani.

**Umaskini**

⇒ Sina sinani, nikiulizwa siungami.
⇒ Abu alisaka kibarua kwa walalaheri na walalahoi.
⇒ Jamaa zake wa karibu walikuwa hohehahe.
⇒ Kijiji kwao walikuwa maskini waliokuwa wakipigiwa mfano.
⇒ Amali nilikuwa fukara wa kutupwa.

**Matumizi ya lugha**

**Utohozi**

⇒ Suti-aliyovaa Abu kujiandaa kwa arusi.
⇒ Motokaa-inayombeba Abu siku ya arusi.
⇒ Hospitali-abu alikotakiwa kufanyiwa uchunguzi Abu kabla ya kusafiri Arabuni.
⇒ Kampuni –ya uchukuzi iliyokuwa imemwajiri huko Arabuni.
⇒ Pasipoti-cheti alichohitaji ili kwenda arabuni.
⇒ <u>Mita</u> mia mbili-nyumba bi arusi alikokuwa kutoka mahali walipoegesha gari.

**Nahau**

⇒ Baada ya kutajirika akaamua kujaribu bahati yake ya <u>kuuasi ukapera</u>-kuoa.
⇒ Sikuwaacha mkono-hakuwapuuza au kuwatenga marafiki zake wa zamani-aliwaajiri.
⇒ Nilikata shauri-pale <u>aliamua</u> kusahau mambo ya kuoa na kuomba Mungu ampe mke mwema ambaye angempenda jinsi alivyo.
⇒ Walikuwa <u>wamefurahi ghaya</u> ya kufurahi-binamu, mdogo wa Abu na jamaa yake kufurahia arusi kupindukia.
⇒ Nimezama katika <u>bahari ya luja</u>-mawazo mengi akiwa garini kuelekea kwa bi harusi.
⇒ Alitimiza mahitaji hayo yote <u>shingo upande</u>-bila hiari/kujilazimisha.
⇒ Mamake kung’ang’ania mtoto wake aandaliwe <u>arusi ya ndovu kumla mwanawe</u>-ya kukata na shoka-kubwa.
⇒ Sikuwa <u>mwenye navyo</u>-tajiri.
⇒ Ilifika mahali fulani nikaamua <u>kupata jiko</u>-kuoa.
⇒ Nilitamauka-kukataa tamaa baada ya posa yake kukataliwa.
⇒ <u>Nilikata shauri</u> kusahau mambo ya ndoa kwa muda-niliamua.
⇒ <u>Usife moyo</u> mwanangu ndoa hupangwa binguni -usikate tama-mjomba baada ya posa kukataliwa.
⇒ Abu alisaka kibarua kwa <u>walalaheri</u> na <u>walalahoi</u>-maskini na matajiri.
⇒ Jamaa zake wa karibu walikuwa <u>hohehahe</u>-maskini.
⇒ Nilikuwa <u>nimeshakata kauli</u>-Abu kuamua kutomwoa amali kwani hampendi ila anapenda mali yake.

**Misemo**

⇒ Sina sinani, nikiulizwa siungami-umaskini

**Chuku**

⇒ Bahari ya kitanda-kitanda kikubwa sana.
⇒ Mlangoni <u>nilikaribishwa</u> na harufu ya manukato <u>iliyozidi kiasi cha kukera pua badala ya kunukia</u>.
⇒ Nyimbo za kina mama kuhanikiza janibu zote.
⇒ Miteteo mitamu yenye uwezo wa kukilainisha chochote hata kiwe kigumu <u>kama</u> almasi.
⇒ Nilikuwa fukara wa kutupwa.
⇒ Kijiji kwao walikuwa maskini waliokuwa wakipigiwa mfano.

**Mbinu rejeshi**

⇒ Jinsi alivyokuwa maskini miaka saba nyuma.
⇒ Alipiga darubini nyuma huko mambo yalikoanzia kiasi cha kujikuta katika hali hiyo-mtanziko-kufikiria kwa kina jinsi alivyopelekwa na mjombake kumposa amali mamake akakataa posa yake.

**Taharuki**

⇒ Nini kinasababisha wasiwasi wa msimulizi?
⇒ Baada ya abu kuondoka shamra shamra za ndoa ziliendelea au zilikoma?
⇒ Sababu ya abu kuvunja ndoa ilijulikana?
⇒ Amali aliolewa au aliendelea kukaa maisha ya ukapera hadi kifo chake?
⇒ Abu alioa mwanamke mwingine au alighairi kabisa kuoa?

**Takriri**

⇒ Wimbo-hongera mwanangu eeh hongera a! Mama uchungu mama uchungu
⇒ Kula kwa taabu, kuvaa kwa taabu-umaskini
⇒ Kupata vitu hivyo nilikuwa <u>nimejikalifu</u> ziada ya <u>kujikalifu</u>-amefipata kwa shida-kifurushi cha majani chai, sukari na marashi.
⇒ Mipango ya ndoa kukamilika hadi kufikia <u>siku</u> ya <u>siku</u>-siku ya arusi.

**Taswira**

⇒ Vitu vingi nyumbani alikuwa amevinunua yeye
⇒ Majilisi ya kiarabu
⇒ Vimeza vidigividogo vya vioo
⇒ Zulia la kiajemi
⇒ Zinga la jokovu
⇒ Runinga kubwa ya rangi
⇒ Bahari ya kitanda
⇒ Godoro kubwa, mito miwili mikubwa
⇒ Shuka za kitanda na foronya zimepigwa darizi

kwa nyuzi za rangi ya dhahabu-tamaa ya Zena.

⇒ Akajijengea chumba cha msonge kilichokandikwa kwa udongo

⇒ Amali haachi ushungi na anavaa mavazi ya sitara(decent)

⇒ Amali kumpelekea orodha ya vitu alivyovitaka kwa ajili ya arusi. Alipendekeza anunue samani kutoka Arabuni, akadai mikufu, pete hata herini, mkoba mzima wa nguo, majora na vitambaa na doto za kanga.

⇒ Mtoto kaumbika si haba! Ukiongeza kujipondoa pamoja na michoro ya hina mikononi na miguuni.

**Tashbihi**

⇒ Uzuri wa amali ulikuwa aula <u>kama</u> hizo pesa-adimu.

⇒ Miteteo mitamu yenye uwezo wa kukilainisha chochote hata kiwe kigumu <u>kama</u> almasi.

**Kinaya**

⇒ Mzee kadiri anataka amali amwondokee nyumbani asije akazalia huko ilhali hakatai msimamo wa mama ambao ulisbababisha bintiye asiolewe.

⇒ Kinaya abu kutoa mali nyingi amwoe amali kisha kumtelekeza siku ya ndoa.

⇒ Kukataa kumwoa ilhali makosa si yake bali amepotoshwa na mamake.

⇒ Kusifu urembo na tabia yake na anaishia kutomwoa ilhali amepotoshwa na mamake.

**Nidaha**

⇒ La hasha!-Abu kukataa hakuwa bahili kwa kutimiza mahitaji ya mama zena shingo upande bali aliuona ni ubadhirifu.

⇒ Abu! Changamka nawe. Hii ni siku yako eti!-binamuye.

⇒ Potelea pote! Liwalo na liwe.

**Tashhisi**

⇒ Amali sidhani kapenda kuolewa nami sikumwoa mimi bali <u>ameolewa</u> <u>na mali yangu</u>.

⇒ Mlangoni <u>nilikaribishwa</u> na harufu ya manukato iliyozidi kiasi cha kukera pua badala ya kunukia.

⇒ Gari letu <u>liliyabinginya</u> masafa polepole

**Mdokezo**

⇒ Wimbo-tuhangaike naye …

**Methali**

⇒ Atafutaye hachoki na akichoka keshapata.

⇒ Ya kesho ajua Mungu.

⇒ Ndoa hupangwa binguni.

**Kejeli**

⇒ Nilipata tetesi alikataa posa yake kwa kuwa hakuwa na uwezo wa kujilisha mwenyewe seuze binti yake.

**Majazi**

⇒ Mzee kadiri-asiye na msimamo.

⇒ Amali-kitega uchumi kama kazi.

**Balagha**

⇒ Mimi si yule waliyenikataa kabla sijenda arabuni?

**Kweli kinzani**

⇒ Abu kutajirishwa na kazi ya uhamali.

**Nyimbo**

⇒ Wa kwanza-bwana arusi ana majukumu mengi.

⇒ Pili-kujifungua si jambo rahisi na mwanamke anapojifungua hupongezwa.

# 11.Tazamana na mauti

⇒ Athari na furaha kupita kiasi/kutojidhibiti kwa furaha kuhusu jambo kwaweza kusababisha hasara-kufurahia ndoto yake kutimia.

⇒ Furaha kumfanya Lucy aendeshe gari bila makini kisha kupata ajali na kuaga dunia.

⇒ Falsafa-usikoke moto kabla ndege hujamtia mikononi.

⇒ Alitembea jiji hilo (London) ili kuliambia kwamba msichana mbichi na tajiri anakuja ili jiji <u>lijitayarishe</u> kumpokea hatimaye. (majivuno)

**Bidii**

⇒ Ya kupata anachokitaka

**Upumbavu**

⇒ Crusoe lulaghaiwa na Lucy kwa urahisi na kuamini kuwa anampenda bila kuchunguza.

**Tamaa**

⇒ Ya kwenda London

⇒ Kuwa tayari kutumia ulaghai kuingia London kama vile kujifanya mtalii, mwanafunzi, mkimbizi, n.k.

⇒ Ya utajiri

⇒ Atafanya kazi za siri kwa vile wanaolipwa mshahara hawaruhusiwi kufanya kazi.

**Unafiki**

⇒ Hampendi crusoe bali anataka kuingia London na kadhalika mali yake.

⇒ Anataka mali anapomtunza.

⇒ Furaha ya Lucy hata kutokwa na <u>machozi ya mamba</u> si shukrani ya dhati.

⇒ Ana hamu ya afe haraka- Hamu ya kutaka mzee yule afe ilizidi maradufu. Angemuua lakini aliogopa sheria.

**Elimu**

⇒ Mtazamo finyu kuhusu elimu

⇒ Haiwafaidi watu sana-haimtajirishi mtu

**Upotoshaji kuhusu maisha ya ulaya**

⇒ Habari –pauni 40 hazitoshi kumtunza msafisha choo kazi ni kung'ang'ania balaa.

**Uhaba wa kazi**
- ⇒ Anajua kwamba hapa pao nchi ya firauni siku hizi hangepata hata hiyo kazi ya tonge la ugali sikwambii muluki.

**Ukengeushi**
- ⇒ kuolewa na mzee.

**Ubahili**
- ⇒ mtu bahili na mtunzaji kama yeye atazizalisha pauni arobaini ziwe elfu arobaini. (chuku)

**Matumaini/kutokata tamaa**
- ⇒ Miaka mingi kupita bila kwenda uingereza lakini hajakata tamaa
- ⇒ Alijiaminisha kuwa kila alichokitaka hukipata
- ⇒ Yeye siku moja ataiona London
- ⇒ Lini ataiona London, hakukata tamaa japo jibu ni gumu

**Matumizi ya lugha**
**Uhuishi**
- ⇒ Alitembea jiji hilo ili kuliambia kwamba msichana mbichi na tajiri anakuja ili jiji lijitayarishe kumpokea hatimaye.
- ⇒ Minyororo ya kufungika kwa hamu ya uingereza ilizidi kuufunga moyo wake-tamaa kuzidi
- ⇒ Ndoto ya lucy ya miaka mingi kupevuka na kujikopoa nje ya akili yake, kuiona imesimama mbele yake kwa dhahiri
- ⇒ Jiko la chini na juu linamwambia mwenzake asogee huko
- ⇒ Huku akiacha tabasamu yake imemganda mzungu moyoni mwake
- ⇒ Kiu ya kuenda London ilikuja kumkaa mioni(kooni) ikamchagiza kama vile kiu ya mtu aliyekuwa akisafiri Jangwani kwa miaka mingi bila kugundua maji

**Tashbihi**
- ⇒ Kiu ya kuenda London ilikuja kumkaa mioni(kooni) ikamchagiza kama vile kiu ya mtu aliyekuwa akisafiri jangwani kwa miaka mingi bila kugundua maji
- ⇒ Lakini wakishafanya hivyo humpita kama upepo wa kibunga na kumwacha yeye mgonjwa wa tamaa
- ⇒ Nguo na mavazi aliyonunuliwa juzijuzi ni kama aliyonunuliwa mwaka mzima

**Utohozi**
- ⇒ Sinema/filamu-alikokuwa akiona Wingereza
- ⇒ Pauni arobaini kwa wiki-mshahara wa mkimbizi uingereza wa juma.
- ⇒ Televisheni, friji-miongoni mwa vifaa ambavyo lucy amesikia wakimbizi hupewa na serikali
- ⇒ Picha zinazotembea-katika filamu

**Kuchanganya ndimi**
- ⇒ Squares-viwanja vya nafasi huko
- ⇒ Love in London-mchezo uliokuwa ukionyeshwa katika filamu

**Balagha**
- ⇒ Kuonyesha ulaghai watu wanaotumia kuingilia mataifa ya magharibi.
- ⇒ Ajifanye mgonjwa mahututi na maradhi yake hayatibiki hapa pao?
- ⇒ Ajifanye anakwenda kusoma?
- ⇒ Tokea lini mtalii mifuko yake iwe mitupu?
- ⇒ Huyo mwanamume kutoka uingereza atakayekuja kumwoa yeye yuko wapi?
- ⇒ Nani atakayetoka uingereza kuja kumwoa yeye?
- ⇒ Vipi Lucy ataingia uingereza?
- ⇒ Kama si peponi huko ni wapi?
- ⇒ Waliosoma anawaona nao wamepata nini?
- ⇒ Kufa kwa mzee huyo si kuko karibu tu?-wakati amechoshwa na siku kusonga polepole.
- ⇒ Lini angepata nafasi ya kupenya kwenye chungio na kudondokea uingereza?

**Taswira**
- ⇒ London barabara zake pana zinazojaa magari na watu pomoni wanaokwenda na kurudi kike kwa kiume vijana na wazee wote waliovaa kifahari na kitajiri maduka mengi yaliyopachanapachana ambayo hujaa bidhaa za kila aina.

**Mdokezo**
- ⇒ Muziki na hasa madisko na sinema…
- ⇒ Pumzi zinanisonga…Crusoe ana ugonjwa
- ⇒ Mtaji mkubwa… unaohitajika mtu awe nao kama anaenda kusoma
- ⇒ Kesho kutwa…waende kwa wakili akaandikishwe utajiri wote wa Crusoe
- ⇒ Akajiona…la hapana…kutoamini angerithi mali yote ya Crusoe.

**Sitiari**
- ⇒ Tama ya kwenda London kuitwa kiu
- ⇒ Wewe umegeuka sungura aliyezikosa zabibu
- ⇒ Ni peponi-uingereza
- ⇒ Eti wanaiita jahanamu-wanaoharibia uingereza jina

**Mbinu rejeshi**
- ⇒ Juzi amemaliza shule ya upili ya juu yaani kidato cha sita lakini hakufaulu vizuri
- ⇒ Hakujali kutofaulu vizuri kwa sababu hakuwa na hamu ya masomo. Hataki riziki kama waliosoma ataka muluki-mali nyingi.

**Nahau**
- ⇒ Kazi yake lucy ni kumkanda na kumsinga mafuta mafuta na mafuta ya mgongo wa chupa

-unafiki

**Takriri**

⇒ Siku ingia siku toka miezi pita miezi rejea-muda mrefu kupita bila kufanikiwa kwenda Uingereza

**Chuku**

⇒ Lucy kumtunza Crusoe mara mbili kama si tatu ya zamani-asikose urithi maana akaribia kufa
⇒ Kumwacha yeye mgonjwa wa tamaa
⇒ Nguo alizonunuliwa juzijuzi tu ni kama alizonunuliwa mwaka mzima
⇒ Viatu havina idadi
⇒ Hawezi hata kutema mate mzee wa watu
⇒ Mtu bahili na mtunzaji kama yeye atazizalisha pauni arobaini ziwe elfu arobaini.

**Sadfa**

⇒ Lucy kuwa na tamaa ya kwenda Uingereza kusadifiana na Crusoe kutokea na kumsaidia kwenda huko-akipanda ngazi kuelekea sinema.
⇒ Akamwahidi angempa zawadi baada ya sinema kwa kumzuia asianguke anaposhikwa na ugonjwa-(shukrani, ukarimu)
⇒ Lucy kuahidiwa kuandikishwa mali na anapoenda mjini hakurudi tena. Kupata ajali na kupoteza roho yake na maiti kuhifadhiwa katika chumba cha kuhifadhia maiti.

**Misemo**

⇒ Watasema mchana na usiku watalala-hawawezi kumwathiri
⇒ Mafuta ya mgongo wa chupa –kujifanya anampenda
⇒ Mapenzi ya kurambishwa asali moja kwa moja kutoka sega la asali.
⇒ Kupaka rangi mbaya uingereza-kuienezea sifa mbaya

**Tafsida**

⇒ Angemlaza-angemuua Crusoe
⇒ Hawezi kumchangamsha kwa namna yoyote
⇒ Ndiyo ni mwanamume asiye na nguvu ya aina yoyote lakini ana utajiri

**Kinaya**

⇒ Crusoe kumshukuru Lucy akidai hajapata kumwona mwanamke mwenye imani kama yeye
⇒ Ana bahati kuliko wazee wote wenye umri kama wake kukutana na msichana mwenye huruma kama yeye
⇒ Kutamaani Crusoe afe haraka kumbe ndiye anatangulia na ndoto yake kushindikana

**Taharuki**

⇒ Baada ya Lucy kufa nani alirithi mali ya Crusoe?
⇒ Alizikwa wapi?
⇒ Siri kwmba hakumpenda Crusoe ilijulikana au alikwenda nayo kaburini ?

# 12.Mwana wa darubini

⇒ Kananda kuomba asaidiwe na darubini kwa kutoweza kukaribia nyumba ya Mwatela amuone Mwakitawa
⇒ Kujiridhisha nafsi yake kwa kumwangalia mtoto wake
⇒ Kananda kumwita mwanawe mwana wa darubini

**Maudhui**

**Utambuaji wa makosa na toba**

⇒ Mwatela kumwandikia Kananda barua ya kumwomba msamaha
⇒ Nimebaini nimekosa mwisho wa kosa
⇒ Katika vita baina ya ubaya na wema, wema daima hushinda
⇒ Angemlipa maovu aliyomfanyia-fidia kwa kumpa nyumba ya kifahari
⇒ Kujitolea kumwelimisha Mwakitawa mpaka afike alikotaka
⇒ Wakili amtafute
⇒ Atie sahihi makubliano-kufuata hatua za kisheria

**Ufarikishaji**

⇒ Kuzuia Mwakitawa wakutane na mamake kudai ni adui na amepanga kumteka nyara adai pesa 2,000,000 amwachilie
⇒ Asipomlipa atamuua
⇒ Achezee nyumbani
⇒ Akampa silaha-kisu na manati

**Adhabu/kisasi kwa maovu**

⇒ Mwatela kufutwa kazi kwa ulevi
⇒ Mtoto wake kufa
⇒ Mkewe kuchomeka
⇒ Kulipa fidia
⇒ Kuugua
⇒ kufa

**Ulevi na athari zake**

⇒ Kupiga mkewe na kusababisha nyumba yake kukosa amani
⇒ Kumbaka yaya wake au kutokuwa mwaminifu katika ndoa/kwa mkewe
⇒ Kufutwa kazi

**Dhuluma dhidi ya wanawake**

⇒ Kananda kubakwa
⇒ Kulaghaiwa
⇒ Kutoroshwa nchi yake
⇒ Kunyang’anywa mtoto
⇒ Kuoza bila hiari kwa mtu asiyempenda
⇒ Kuuzwa utumwani

**Migogoro**
⇒ Kupiga mkewe wakati wa ugomvi
⇒ Basi mwite mwakitawa sasa hivi na umwambie ukweli kwamba alikuwa anaua mama yake mzazi

**Ubwana na utwana**
⇒ Bwana na bibi Mwatela walimwajiri Kananda kama yaya

**Umaskini na athari zake**
⇒ Wazazi wa Kananda walikuwa miongoni mwa akina pangu pakavu waliokuwwa umma mkubwa nchini
⇒ Wazazi wa Kananda kushindwa kumpeleka shuleni
⇒ Kusababisha kananda aendelee kufanya kazi kwa Mwatela na kumsababishia madhila
⇒ Kushindwa kusaidia Kananda kudai haki kupitia vyombo vya sheria

**Imani kwa Mungu**
⇒ Kananda kuendelea kumwomba Mungu siku moja amwonee huruma amkutanishe na mwanawe
⇒ Aliamini siku moja Mungu angemkutanisha na mwanawe

**Mapenzi ya dhati**
⇒ Kananda kwa mwanawe
⇒ Kujitahidi kumtafuta
⇒ Ami yake mbao kusaidia kananda kupata darubini
⇒ Mwatela kuendelea kumpenda mkewe hata baada ya kuchomeka na kuharibika sura
⇒ Upendo wa maria kwa mumewe kwa kuvumilia ulevi na uzinifu wake
⇒ Kukaa naye hata baada ya kufukuzwa kazi na kuishi kwa shida
⇒ Kumsamehe kwa kuzaa nje ya ndoa

**Ujasiri**
⇒ Kupigania haki ya kumuona mwanawe

**Subira na ustahimilivu**
⇒ Kuchukua muda mrefu wa kumwangalia mwanawe

**Uoga**
⇒ Kumwogopa Mwatela na kuamua kumwangalia mtoto kwa darubini

**Nafasi ya mwanamke katika jamii**
⇒ Maria ni mkombozi
⇒ Ni punda wa huduma
⇒ Ni jasiri
⇒ Hakati tama
⇒ Ni chombo cha mwanamume cha kujiburudisha
⇒ Amenyimwa elimu
⇒ Ana sauti/usemi
⇒ Mvumilivu
⇒ msamehevu

**Ukarimu**
⇒ Mbao kujitolea kuuza kuku na mbuzi ili kupata pesa za kumnunulia Kananda darubini-kujali maslahi ya wengine

**Bidii**
⇒ Mwatela kuanza biashara na kutajirika

**Ukweli**
⇒ Maria kumwambia Mwakitawa ukweli kuhusu mamake

**Ujirani mwema**
⇒ Jiraniye Mwatela kumshauri kupiga ripoti polisi kuhusu mama mwenye darubini

**Mabadiliko**
⇒ Mwatela kufutwa kazi
⇒ Kuacha ulevi na kuanza biashara ya uvuvi na kuuza samaki
⇒ Kutajirika
⇒ Mkewe kuwa mwalimu

**Udanganyifu na athari zake**
⇒ Nusura Mwakitawa amuue mama yake kwa kumdanganya ni adui
⇒ Mwatela kuishi kwa wasiwasi akihofia angejulikana
⇒ Ugonjwa wa shinikizo la damu kwa kuwaza sana namna ya kuficha ukweli
⇒ Kulazimika kulipa fidia Kananda kwa yote aliyomtendea
⇒ Mwatela kumkosa mtoto wake wa pekee kwa kutotaka kuishi tena na babake kwa ulaghai aliomfanyia
⇒ Mtoto kudanganywa mama yake alikufa alipozaliwa
⇒ Mwatela kupeleka ujumbe kwa wazazi wa Kananda kwamba mwanao alitoweka na hakuna aliyejua alikotorokea
⇒ Hakumwoa kananda kama alivyomwahidi
⇒ Amwambie mama Sami mimba ni ya rafiki yake wa huko nyumbani kwao.

**Tanzia**
⇒ Moto kuua watu watano-watoto wawili na watu wazima watatu
⇒ Maria kuchomeka vibaya
⇒

**Matumizi ya Lugha**

**Mbinu rejeshi**
⇒ Kananda alizaliwa wakati wa enzi ya ukoloni nchini Kenya
⇒ Uhuru ukitangazwa alikuwa na umri wa miaka kumi na mine
⇒ Wazazi wa kananda walikuwa maskini na

hawakuweza kumsomesha alikaa nyumbani
- ⇒ Jioni ulevi ulimtuma Mwatela kumtia doa Kananda
- ⇒ Usiku Kananda alipata maumivu ya kujifungua uliotokea mkaza wa moto

**Utumwa**
- ⇒ Dereva kuishi na Kananda kwa miezi kadha kabla ya kumuuza kama mtumwa kwa mtu mwingine

**Nahau**
- ⇒ Alipanga njama ya kinyama-kumnyang'anya kananda mtoto na kupanga na dereva wa malori makubwa ya Kongo amchukue amfanye mkewe
- ⇒ Kumtia moyo-kumletea habari za kumpa matumaini ya kumpata mtoto wake kuwa mwatela alihamia Mombasa na mwanao
- ⇒ Yu hali mahututi-aliporudi kutoka hospitalini
- ⇒ Nitakutoa roho-angemuua angemwambia mke wake
- ⇒ Kumtia doa Kananda-kumbaka mkewe alipotembelea wazazi wake
- ⇒ Kichapo cha mbwa-kikali
- ⇒ Jaribio la mama Sami kujiokoa liligonga mwamba-lilishindwa
- ⇒ Walifurahi ghaya
- ⇒ Hasira za mkizi-zinazomletea mtu hasara
- ⇒ Wazazi wake walikuwa miongoni mwa akina pangu pakavu waliokuwwa umma mkubwa nchini-maskini hangeweza kusomeshwa kwa sababu ya uchochole wao alikaa nyumbani
- ⇒ Bwana mwatela alipenda kuchapa mtindi-kunywa pombe
- ⇒ Wazazi wa kananda walifurahi ghaya -sana hadi upeo wa furaha

**Kuchanganya ndimi**
- ⇒ <u>Kampuni</u> ya simba <u>breweries</u>-anakofanya kazi Mwatela
- ⇒ Oh my god! Mwakitawa! Mwakitawa! Njoo haraka baba yu taabani!
- ⇒ Benjamin, please don't die

**Utohozi**
- ⇒ Kampuni

**Misemo**
- ⇒ Kweli mungu hamtupi mja wake
- ⇒ Hulka ya mtu haifichiki kwa muda mrefu.
- ⇒ Kumbe ile asali chungu ilizaa karaha-mimba
- ⇒ Kananda alilala maskini akaamka tajiri
- ⇒ Kumbe maisha ni fumbo-barua kwa kananda

**Tashhisi**
- ⇒ Jioni ya siku hiyo ulevi wa mwatela <u>ulimtuma</u> kumtia doa kananda
- ⇒ Ulevi huu <u>ulimpeleka</u> bwana Mwatela katika ngazi nyingine-kumchokoza kananda kwa kumtaka mapenzi
- ⇒ Kimya chake kikawa <u>kinamchoma</u> ndani kwa ndani

**Chuku**
- ⇒ Alilia usiku na mchana

**Balagha**
- ⇒ Uniulie nini na ndoa yetu na wewe inamhusu pia yeye?
- ⇒ Nilikuwa namuua mama yangu?
- ⇒ Mamangu yupi?
- ⇒ Nimuue kwa nini?
- ⇒ Ungemwambia ukweli upi isipokuwa ule niliomwambia?

**Uzungumzi nafsia**
- ⇒ Mbona Benjamini Mwatela aliniambia mama yake Mwakitawa alifariki?

**Sadfa**
- ⇒ Usiku mmoja wa manane kananda kupatwa na maumivu ya kujifungua na usiku uo huo moto kuzuka katika nyumba ya jirani ukaenezwa na upepo na nyumba ya mwatela na kuangamiza mtoto na kumchoma mama vibaya.
- ⇒ Mwatela kupelekwa hospitalini alikokuwa amelazwa kananda
- ⇒ Mwakitawa kutoweka kwa siku nne

**Tabaini**
- ⇒ Wazazi wa kananda wakisaidiwa na mbao waliuza vitu vidogovidogo <u>si</u> mbuzi <u>si</u> kuku ili wapate pesa za kununulia darubini

**Taharuki**
- ⇒ Mwakitawa alipotoweka kwa siku nne alikuwa wapi?
- ⇒ Mama angepona baada ya kuchomeka vibaya?
- ⇒ Mwatela kweli angemuoa?
- ⇒ Wangefaulu kupata darubini?
- ⇒ Kananda angefaulu kumtoa mwanawe mikononi mwa Mwatela?

**Nidaha**
- ⇒ Mariaa! Kwani hungeweza kusubiri nitoke hospitalini nimwambie mimi mwenyewe?
- ⇒ Oh my god! Mwakitawa! Mwakitawa! Njoo haraka baba yu taabani!
- ⇒ Benjamin, please don't die

**Methali**
- ⇒ Mungu si athumani

**Taharuki**
- ⇒ Mwisho wa Mwatela ulikuwaje?
- ⇒ Je alipata mtoto mwingine au alikufa bila mtoto?
- ⇒ Mwatela na maria walihamia wapi baada ya kumkabidhi kananda nyumba?

## 13.Mizizi na matawi

- ⇒ Sitiari-mtoto asiye na wazazi wawili hupata shida kama vile miti hupata ikikosa mizizi na matawi
- ⇒ Watu huweza kupoteza mizizi na matawi yao lakini bado akabaki mtu
- ⇒ Mama Sudi alikuwa ni mizizi na baba Sudi alikuwa ni matawi

**Maudhui**

**Nafasi ya mwanamke**

- ⇒ Mlezi mzuri-mama Sudi kumpa malezi mazuri
- ⇒ Mpatanishi

**Athari ya maisha yasiyo ya uadilifu ujanani**

- ⇒ Mimba nje ya ndoa
- ⇒ Kutupa mtoto
- ⇒ Kuteseka kwa kumkosa mtoto-umaskini kwa kukosa msaidizi
- ⇒ Athari za kisaikolojia

**Upatanishi**

- ⇒ Sudi mwanangu naomba usahau yote yaliyopita umpokee Bi. Kudura uwe naye kwa hali na mali kuliko hata vile ulivyokaa na mimi-hana ubinafsi (mkweli)

**Anasa/starehe na athari zake**

- ⇒ Sudi ana wapenzi kadha-Waridi na Ridhaa
- ⇒ Mamake halisi Bi. kudura alimtupa ili aendelee na anasa

**Udanganyifu**

- ⇒ Sudi kuitwa jina lisilo na uhusiano na la babake wala ukoo wake
- ⇒ Kumdanganya babake ni Sudi bin Abdalla
- ⇒ Vile walioana kwa mapenzi makubwa
- ⇒ Vile alifariki
- ⇒ Uongo wa mamake ulibainika-njia ya mwongo ni fupi

**Ukarimu**

- ⇒ Kumwokota na kumlea
- ⇒ Kutokana na ukarimu wa sudi wa kumwajiri Bi. Kudura anakuja kumpata mamake halisi.

**Heshima**

- ⇒ Sudi hakutaka kumtuma kudura kwa kumwona amemzidi umri

**Umuhimu wa mtoto**

- ⇒ Ukitaka kujua hasara za kukosa mtoto tazama faida za mwenye mtoto

**Utambuaji wa makosa na kutubu**

- ⇒ Anamuomba Mungu amsamehe

**Elimu**

- ⇒ Sudi kusomea shahada ya juu ya udaktari wa sheria nchini moja ulaya

**Heshima/mapenzi kwa wazazi**

- ⇒ Kumwajiria mtumishi

**Matumizi ya lugha**

**Balagha**

- ⇒ Nani?-hakuna aliyekosa kujua kuhusu mapenzi yao
- ⇒ Bila shaka ungemuita asingekataa kuitika na kwa nini akatae?
- ⇒ Mara ngapi Sudi amekuwa akimuuliza mama yake habari za baba yake?
- ⇒ Mwanangu tangu lini kipwendacho kikadumu?
- ⇒ Inakuwaje mtu akiambiwa yeye ni kiumbe wa kuokotwa?
- ⇒ Husimamaje?
- ⇒ Huendaje katika dunia ya masuto na nazaa matusi aibu na fedheha?
- ⇒ Atafayaje Sudi?
- ⇒ Furaha yangu itoke wapi tena?
- ⇒ Kwa nini mama yake amfiche?
- ⇒ Kwa nini asimwambie ukweli?
- ⇒ Au apige moyo konde afichue siri?-ajikaze kufanya jambo gumu-kusema ukweli
- ⇒ Hapa alipo mayai yamemuisha mtoto angetoka wapi?
- ⇒ Angemuambia tu mwenyewe akajua maana kama uharamu utakuwa wa mtoto, kosa la nani?

**Nahau/misemo**

- ⇒ Yaliyopita huwa yamepita nasi huwa hatuna uwezo wa kuyarejesha.
- ⇒ Dunia kuna mambo na katika hayo mambo kuna majambo-maajabu
- ⇒ Mamake alikwisha mtengenezea kiamsha kinywa-chakula au kinywaji cha asubuhi
- ⇒ Hunipeleka mbali ya siku zile za asali na maziwa.
- ⇒ Ndio Kudura huja tukaondoka-tunazaliwa na kufa
- ⇒ Mahali pa kuweka ubavu-Sudi mamake awe akimpa mtumishi mahali pa kulala
- ⇒ Atauliza tu ajue moja-mbivu au mbichi-ukweli na uongo wa mambo
- ⇒ Kukata tamaa-kupoteza matumaini ya kumjua/kumwona babake
- ⇒ Suti aliyovaa ilimtoa akatoka
- ⇒ Mapenzi yangu kwake yakazidi mno tangu alipoingia ndani-yaani aliponioa
- ⇒ Ndipo nami nikampenda kufa na kupona
- ⇒ Tukapendana kwa moyo mmoja
- ⇒ Kuna kupata na vile vile kukosa

⇒ Ajue asili na fasili yake-alitaka kumjua babake
⇒ Kupiga deki

**Mdokezo**

⇒ Ndiyo…maana hata mwenyewe hakuwa na uhakika na uhakika wa jina Lake.
⇒ Basi akawa akiitwa Sudi … Sudi Abdalla

**Methali**

⇒ Kipendwacho hakidumu
⇒ Damu iliyo daima nzito kuliko maji
⇒ Nguvu za maji ni mawe mlimwengu ni mwanawe
⇒ Kuvyaa kupoma-mamake kukumbuka kauli ya wahenga
⇒ Mungu akuwekavyo ndivyo ukaavyo-majaaliwa
⇒ Mungu akikupa kilema hukupa na mwendo

**Tashbihi**

⇒ Sudi alikuwa anamuona babake <u>sawa</u> na mhusika wa hadithini-kwa mawazo tu
⇒ Kila siku n'na jambo n'nataka n'kuulize lakini ulimi mzito <u>kama</u> nanga
⇒ Nilimlea mwenyewe naye akakua kama mgomba
⇒ Wote wakalizana kama waliofiwa
⇒ Kwa sudi maneno hayo <u>yalikuwa</u> msumeno butu unaokeketa kwa maumivu makali-yakimchoma sana
⇒ Mama mtu hujaribu kumtuliza na sudi hutulia japo si kama maji ya mtungi-hatulii kabisa

**Takriri**

⇒ Maneno yake daima yalikuwa hayo hayo
⇒ Abdalla baba yako-Abdalla bin Sudi

**Mbinu rejeshi**

⇒ Mamake hakufanikiwa kupata mtoto
⇒ Mungu akampa mtoto mzuri wa kiume kwenye pipa la taka
⇒ Akashukuru mungu
⇒ Akamlea vizuri
⇒ Akakua kama mgomba, mnazi unachelewa
⇒ Akamsomesha
⇒ Mtumishi kusimulia kuhusu mtoto aliyemzaa nje ya ndoa
⇒ Alikitumbukiza katika pipa la taka
⇒ Sudi kukumbuka karamu ya siku kuu ya pasaka jinsi walivyokuwa na Waridi kutoka Afrika Kusini - Gaboron

**Chuku**

⇒ Sudi alikuwa amewaniwa na kila mwanamke
⇒ Dunia yote ikawa yao na kila mtu ametosheka
⇒ Tokea kifaranga hadi kuku kila mtu alijua kuhusu mapenzi ya mamake na babake
⇒ Baba yako alinipenda bila ya kikomo
⇒ Tangu hapo nikawa mkiwa tena wa maisha

**Tashhisi**

⇒ Msiba mkubwa ukainiangukia-kifo cha mmewe bandia
⇒ Mkonyezo ulikoleza hamu katika noyo za vijana hata wasipate kukumbuka kilichowaleta ughaibuni
⇒ vyote hivyo vikaonekana kushiriki kikamilifu katika dhifa ile
⇒ Sudi alipiga gari lake moto na taratibu likatambaa na kuanza kuyabungunya masafa kuelekea lilikokusudiwa
⇒ Tea breeze-walevi walikuwa <u>wakizungumza</u> na chupa zao za pombe
⇒ Mara Sudi akalipiga mkwaju-alielekea na gari likatimka kuelekea benki
⇒ Ndipo kudura <u>ilipomsaka</u> na <u>kumshika</u> mkono na kisha <u>kumuongoza</u> hadi ilipo damu yake.
⇒ Dunia ina rai zake
⇒ Kwa yule mtumishi wao yalimchoma kwa woga na wasiwasi
⇒ Bado nguvu ya shetani ikimtonesha kwa <u>kumwambia</u> mambo yangekuwa mazuri kama angekuwa na yai lake mwenyewe
⇒ Siku <u>hazikusimama</u>-zilikutwa zikachwa na maisha yakapungua na kuyoyoma
⇒ Alimkuta radhia ambaye alikuwa kachoka <u>kugombana</u> na wakati-kumngojea

**Taswira**

⇒ Sudi alikuwa kijana mwembamba, mrefu kwa kimo chake, mtanashati
⇒ Suti aliyovaa ilimtoa akatoka

**Kuchanganya ndimi**

⇒ wasichana kumuita <u>handsome</u>
⇒ Easter get together-karamu ya siku kuu ya pasaka
⇒ Karamu ilifanyika katika hoteli ya <u>royal palm</u>

**Anasa/starehe**

⇒ Ukumbi ulivuma kwa mtu na muziki, seuze machupa ya soda bia mvinyo na vinywaji vingine kemkem?
⇒ Watu <u>wawili wawili</u> mwanamume na mwanamke

**Utohozi**

⇒ Bosi-Bi. Kudura anavyomwita mama Sudi.
⇒ Tibirinzi-Tea Breeze-anasa-wacheza ngoma watoto kustarehe kwa bembea <u>treni</u> farasi n.k.
⇒ Walevi <u>madensi madisco</u>

**Tanakuzi**

⇒ Sudi na Radhia Tea Breeze Wakatazamana na <u>kufurahi</u> palipofurahisha <u>wakahuzunika</u> palipohuzunisha

⇒ Mlikuwa mseto wa furaha na huzuni

**Koja**

⇒ Yeye atakuwa akikusaidia kazi zako zote za nyumba-kupika, kufagia, kupiga deki (kupangusa na kusafisha sakafu, kufua na kila kitu.

**Tanakali**

⇒ Kauli yake haikutoka ng'o-mamake Sudi kwa kusikia kuhusu mtoto wa mtumishi anashindwa kusema

⇒ **Sadfa**

Sudi kumpa Kudura ajira bila kujua na kutokea kuwa ndiye mamake

**Tabaini**

⇒ Si sudi, si bimkubwa na wala si Kudura

**Taharuki**

⇒ Sudi alisemaje baada ya kufahamu mamake halisi?

⇒ Alimkubali mamake aliyemtupa?

⇒ Alimkubalia mamake mlezi aondoke?

**Takriri**

⇒ Basi watu walicheza mpaka wakacheza tena wakafurahi na wapenzi wao hata wakasahau matatizo yao